SPORTPESA APP

CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA



PAKUA SASA




**Achinjwa** nyumbani kwa baba yake usiku kwa deni la 400,000/-

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Septemba 6, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580695

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## SAKATA MGONJWA KUFUMULIWA NYUZI:

# Waziri atoa siku 10 kupata majibu

UKURASA 2



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede (wapili kulia), akimkabidhi Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, sehemu ya mchango wa rimu za karatasi 1,500 na taulo za kike ikiwa ni msaada kutoka benki hiyo kwa ajili ya kuboresha elimu jijini Dodoma. Kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna. **Habari Uk. 15. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 2

## SADC YAIPATIA TANZANIA MIL. 600/- KUSAIDIA WAZEE

JUMUIYA ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), imeipatia Tanzania zaidi ya Sh. milioni 600 kusaidia huduma za wazee wasiojiweza nchini.

Fedha hizo ni sehemu ya mradi wa kusaidia huduma za wazee katika nchi tatu zikiwamo Malawi na Msumbiji...

UKURASA WA 3

## ASKOFU GWAJIMA ANENA SAMIA KUTANGAZA UTALII

MBUNGE wa Kawe, Askofu Josephath Gwajima, amesema kazi inayofanywa na Rais Samia ya kujitolea kutengeneza vipindi maalum vya kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania, ni ya kuungwa mkono na kila mtu.

Askofu Gwajima alitoa...

# Sasa rukhsa kuchanganya chanjo za corona

UKURASA 4






# Rais Samia kuitangaza tanzanite kimataifa

UKURASA 2


**MICHEZO** NABI ATOA AGIZO ZITO KWA DIARRA, AUCHO UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

## SADC yaipatia Tanzania mil. 600/- kusaidia wazee

**Na Faustine Feliciane**

JUMUIYA ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), imeipatia Tanzania zaidi ya Sh. milioni 600 kusaidia huduma za wazee wasiojiweza nchini.

Fedha hizo ni sehemu ya mradi wa kusaidia huduma za wazee katika nchi tatu zikiwamo Malawi na Msumbiji.

SADC imetoa pesa hizo kwa Tanzania kupitia Taasisi ya HelpAge ambayo imejikita kwenye kusaidia wazee katika masuala mbalimbali ikiwamo afya.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wakifunga semina ya siku mbili iliyowakutanisha taasisi zilizopokea pesa hizo kutoka Tanzania, Msumbiji na Malawi, Mratibu wa programu hiyo kutoka HelpAge, Dk. Edwin Mung'ong'o, alisema fedha hizo ni za kusaidia huduma za wazee na programu hiyo inafanyika katika Mkoa wa Tanga kwenye wilaya za Lushoto na Handeni.

"Wazee wana changamoto zao katika maisha ya kila siku changamoto kuu tatu ni huduma za afya rafiki, upatikanaji wa kipato kumwezesha kukidhi mahitaji yao, pia usalama wao, SADC wameliona hili na hizi pesa ni kwa ajili ya kusaidia katika nyanja hizo, HelpAge itatoa elimu kwa waelimishaji na wasaidizi wa wazee ili kuwapa huduma zinazopaswa kwa wazee," alisema Mung'ong'o.

Alisema programu hiyo ni ya miaka miwili na Tanzania imepata fursa hiyo kwa mara pili mfululizo.

Mradi huo kwa mara ya kwanza ulifanyika kwenye nchi za Tanzania, Afrika Kusini na Zimbabwe na sasa inafanyika kwa awamu ya pili huku Tanzania ikiwa kinara kwenye mradi huo.

"HelpAge inashirikiana kwa karibu na Tume ya Ukimwi Tanzania (TACAIDS) kwa sababu kundi la wazee limerukwa kwenye masuala ya afya ikiwamo afya ya kujikinga na kuishi na Ukimwi...," alisema Dk. Mung'ong'o.

Katika mgao huo wa pesa za SADC katika mradi huo wa awamu ya pili Msumbiji imepewa Sh. milioni 255 huku Malawi ikipewa milioni 214.

Mradi huo utafikia tamati mwaka 2023.

# Waziri Gwajima atoa siku 10 mgonjwa kufumuliwa nyuzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUKIO la tabibu wa Zahanati ya Kerenge, Kata ya Kibaoni, wilayani Korogwe, kudaiwa kumfumua nyuzi majeruhi wa ajali ya pikipiki limemwibua Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ambaye ametoa maagizo kuhusu tukio hilo. Tabibu huyo, Jackson Meli, anayetuhumiwa kumfumua nyuzi majeruhi, Zubeda Ngereza aliyapata ajali ya pikipiki Julai 28, mwaka huu na kupelekwa katika zahanati hiyo, kushindwa kulipa gharama ya matibabu Sh. 10,000.

Tukilo hilo ambalo video yake ilisambaa katika mitandao ya kijamii juzi ilizua gumzo na maswali kadhaa juu ya undani wa tabibu huyo kudiriki kuchukua uamuzi huo.

Video hiyo ilimwonyesha tabibu huyo akikiri kufanya tukio hilo mbele ya Diwani wa Kata ya Kerege, Abdallah Robo, aliyekuwa akimhoji. Akieleza kwamba alitaka kulipwa gharama za matibabu.

Taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Habari cha Wizara hiyo jana, ilimnukuu Waziri Gwajima akitoa agizo kwa mabaraza yote ya kitaalamu yanayohusika na usimamizi wa huduma za afya nchini yafike katika Halmashauri ya Korogwe kuchunguza tukio hilo, kuchambua mfumo mzima wa utoaji huduma kwa wagonjwa, ili kubaini hali halisi na kupanga hatua stahiki.

Kupitia taarifa hiyo, Waziri Gwajima alisema: "Mabaraza yote ya kitaalamu yanayohusika na usimamizi wa huduma za afya nchini yanapaswa kwenda kuchunguza tukio hilo ili kubaini hali halisi na kupanga hatua stahiki za kuchukua kuhusu sakata hilo".

Mbali na kueleza hayo, Dk. Gwajima pia alitoa siku 10 taarifa ya tukio hilo iwe imekamilika na kuwasilishwa mezani kwake.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, Halfani Magani, alikiri kuwapo kwa tukio hilo, kwamba tabibu huyo alishaondolewa katika zahanati hiyo, aliwapokea majeruhi hao na kuwapa huduma.

Alisema halmashauri hiyo ilipokea taarifa hizo na kwa kushirikiana na polisi walimkamata tabibu huyo ambaye alikaa chini ya uangalizi katika Kituo cha Polisi Korogwe kuanzia Julai 28 hadi 30, mwaka huu, kisha alisimamishwa kazi na kumpatia hati ya mashtaka kwa kuzingatia kanuni za utumishi wa umma. Magani alisema huduma ambazo aliwapatia zilikuwa pamoja na kumshona mama huyo nyuzi katika eneo la mkono na kumfunga bandeji na dereva wa bodaboda alifungwa bandeji maeneo aliyoumia.

Kwa mujibu wa Magani, baada ya huduma hiyo ndipo tabibu alipodai gharama za matibabu ambazo kwa huyo mama zilikuwa ni Sh. 10,000 na aliposhindwa kulipa kwa wakati huo, akafanya uamuzi wa kumfumua nyuzi.

# Rais Samia kuitangaza tanzanite kimataifa

**Na Godfrey Mushi, HAI**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema kilio cha muda mrefu kuhusu madini ya tanzanite kutojulikana kuwa yanapatikana kwa upekee nchini kinakaribia kumalizika.

Akizungumza jana alasiri na wakazi wa Bomang'ombe katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai mkoani Kilimanjaro, Rais Samia, alisema anachokifanya kwa sasa ni kutengeneza filamu itakayoonyesha mazuri yaliyopo nchini.

"Tumekwenda Mirerani (Simanjiro) kuuonyesha ulimwengu kwamba tanzanite ni ya Tanzania. Tumekwenda kwenye machimbo, tumechukua namna inavyochimbwa, inavyopimwa, inavyoongezwa thamani mpaka tunapata vito.

"Sasa wale wanaouza ovyo ovyo huko, wajue hiyo kitu kwao ni Tanzania. Na ulimwengu utaamini hivyo, kwa sababu sisi tunawaonyesha, lakini kubwa zaidi kuitangaza tanzanite yetu ili zisizagae duniani ovyo ovyo," alisema Rais Samia.

Aidha, alisema baada ya kutoka Mirerani anaelekea kwenye Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro kwenda kupiga picha na kuonyesha mlima huo uko Tanzania.

"Huko duniani wengine wanaamini Mlima Kilimanjro uko nchi jirani. Tunakwenda kuupiga picha na kuuonyesha kusema uko ndani ya Tanzania. Sasa hivi tunaelekea Marangu ambako tunakwenda kupanda mlima kidogo, tuchukue picha, kwa sababu picha ya mlima tulishachukua. Halafu jioni kabisa tutakwenda Ngorongoro.

Leo (kesho) Rais Samia na msafara wake wataendelea na ziara yake ya kurekodi vivutio vya utalii maarufu kama Royal Tour katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na maeneo yote ya Tanzania ambayo yana vitu maalum vya kuuonyesha ulimwengu.

Akiwa Bomang'ombe, Rais Samia alisema: "Kwa vile nimewakuta hapa nizungumze kidogo yale ninayoyajua kwenu. Sijamaliza tatizo la maji ndani ya Bomang'ombe, najua. Tuna mradi mkubwa tunaupanga na Halmashauri ya Hai. Mradi wa shilingi bilioni moja kuhakikisha kwamba tunaleta maji maeneo yaliyobaki ndani ya Bomang'ombe.

"Najua kwamba ndani ya Hai, kuna mgogoro wa ardhi unaohusisha Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA), mgogoro na wenyewe tunaushughulikia.

"Tunachokifanya sasa ni kukusanya vielelezo vya wote walioko kwenye eneo na tuone nani alikuwapo kihalali lakini kila mwenye haki anakwenda kupata haki yake."

Mgogoro huo wa ardhi, unawahusisha wananchi wa Kata ya KIA na Kampuni ya Uendeshaji na Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA).

Rais Samia alisema Desemba mwaka huu anajipanga kuanza ziara yake nchi nzima na atarejea Kilimanjaro kwa ziara rasmi.

Kuhusu tatizo la miundombinu ya Soko la Kwa Sadala, Rais Samia alisema anajua kwamba soko hilo ni dogo.

"Wajasiriamali oyee! Na ndiyo wengi mlioko hapa soko lile ni dogo, najua Bomang'ombe ina kama wafanyabiashara 1,000 hivi, lakini soko lile linachukua watu 100.

Rais Samia alisema: "Kwa hiyo serikali yenu tunajipanga kujenga soko jipya kule eneo la Mashine Tools. Tutajenga soko lingine ambalo wale ambao hawataingia Bomang'ombe watakwenda kuingia huko. Tunakwenda kufanya kazi na halmashauri yenu ili tuondoshe changamoto hiyo.



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai na Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) kwa ajili ya kuendelea kurekodi kipindi maarufu ya Royal Tour jana. **PICHA: IKULU**

# M'biashara afikishwa kortini madai kubaka

**Na Thobias Mwanakatwe**

MFANYABIASHARA wa mjini Kyela, Bush Mwalusako, aliyekuwa akituhumiwa kutorosha wanafunzi wa sekondari, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, akikabiliwa na shtaka la kubaka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Urlich Matei, akizungumza na gazeti hili alisema mfanyabiashara huyo ambaye alikamatwa mwishoni mwa mwezi uliopita, amefikishwa katika mahakama hiyo juzi (Ijumaa) na kufunguliwa kesi namba 40 ya mwaka 2021.

Alisema kesi hiyo ambayo ipo kwa Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mbeya, Andrew Peter Scout, itakuja kwa hatua ya kutajwa Septemba 13, mwaka huu, katika mahakama hiyo na mtuhumiwa yupo nje kwa dhamana. Mfanyabiashara huyo alikamatwa eneo la mpaka wa Namanga, mkoani Arusha mwishoni mwa mwezi uliopita akiwa na mwanafunzi mmoja ambaye ni kati ya wawili aliodaiwa kuwatoroshwa.

Tuhuma za kutoroshwa wanafunzi hao katika tukio lililotokea Januari mwaka huu, ziliripotiwa katika Kituo cha Polisi Kyela Mjini na kupewa RB namba KY41/RB/07/2021 na katika kituo kidogo cha Osaka na kupewa RB namba ISK/RB/41/2021.

Kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo kumechochewa na ufuatiliaji wa karibu uliokuwa ukifanywa na maofisa wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na taarifa zilizokuwa zikitolewa mara kwa mara kwenye gazeti la Nipashe kuhusiana na tukio hilo.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mpindimbi Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, wakishika mashine za vyerehani vya kushonea taulo za kike (SODO) vilivyotolewa kama msaada na Taasisi ya Haki Elimu kwa baadhi ya shule za msingi na sekondari wilayani humo jana.
**PICHA: HAMISI NASR**

# Achinjwa nyumbani kwa baba yake usiku kwa deni la 400,000/-

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

MKAZI wa Majengo Sokola, katika Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, Gongo Charles (30), ameuawa kwa kuchinjwa na watu wanaodaiwa kumdai Sh. 400,000.

Kwa mujibu wa baba mzazi wa marehemu, Charles Kwilasa, tukio la kuuawa mwanawe limetokea Agosti 4, mwaka huu, usiku.

"Majira ya saa mbili usiku tulipomaliza kula chakula familia nzima tukaingia kulala akiwamo marehemu, kumbe kijana wangu baadaye alitoka nje na baada ya kufika saa tano akaja kwenye dirisha la nyuma kumgongea mdogo wake," alisema.

Kwilasa alisema, mdogo wake wakati anamfungulia kaka yake alikuwa na watu wawili na alipoingia ndani walianza kudaiana pesa.

Aliwanukuu wakisema; "tupe sasa hela zetu tuondoke". Alisema kwa kuwa hakuwa na chochote aliingia chumbani kwenda kumwomba mdogo wake ambaye naye alimweleza hana kiasi chochote bali kiasi alichokuwa nacho tayari amenunua mchele.

Mzazi huyo aliendelea kusimulia kuwa vurugu zilianzia hapo wakati yeye hakujua kinachoendelea, lakini baada ya kusikia mwanawe akilia ndipo alipofungua mlango wake na kutoka nje na alikutana watu wawili wakitoka nje haraka.

Aliendelea kusimulia kuwa kabla ya kuwafuatilia alifika mdogo wake na kumweleza kuwa kaka yake amepigwa na kucharangwa mapanga na watu wawili.

Kwa mujibu wa maelezo ya mzazi huyo wauaji baada ya kukosa kiasi wanachotaka na kabla ya kutekeleza mauaji hayo walimtaka marehemu akaombe kiasi hicho kwa baba yake.

Alisema hata hivyo, alikataa na kuwaahidi kuwa angewalipa baadaye ndipo watu hao walipopandwa na hasira na kumfanyia ukatili huo. Mdogo wa marehemu, Derick Charles, akizungumza na gazeti hili nyumbani kwao, alidai kuwa majira ya saa tano usiku aligongewa dirisha na kaka yake na alipokwenda kufungua mlango alirudi kulala, lakini baada ya muda mfupi kaka yake alimfuata chumbani na kumwomba kiasi cha Sh. 400,000 ili awakabidhi watu wawili aliofika nao ndani kwa madai kuwa wanamdai.

"Mimi nilimwambia kaka kwa sasa sina hela bali nimezinunua mchele kwa ajili ya kuuza kwenye kibanda changu baada ya kumweleza hivyo alirudi sebuleni na kulala."

Alisema alimwambia kaka yake ambaye kwa sasa ni marehemu azime taa na kufunga mlango, lakini hakumjibu chochote.

Muda mfupi baadaye alisema akasikia kelele za kuomba msaada na alipotoka chumbani alikuta akiwa ashafariki kwa kuchinjwa na kucharangwa mapanga sehemu mbalimbali za mwili wake," alisema Derick. Derick alisema baada ya kushuhudia mauaji hayo wauaji walitokomea kusikiojulikana na aliamua kutoka nje ili kumweleza baba yake jinsi tukio lilivyotokea.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kuongeza kuwa wanaendelea na msako ili kuwabaini watu waliofanya unyama huo.

# Askofu Gwajima amfagilia Rais Samia kutangaza utalii

**Na Elizabeth Zaya**

MBUNGE wa Kawe, Askofu Josephath Gwajima, amesema kazi inayofanywa na Rais Samia ya kujitolea kutengeneza vipindi maalum vya kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania, ni ya kuungwa mkono na kila mtu. Askofu Gwajima alitoa kauli hiyo jana akiwa kwenye ibada kwenye kanisa analoliongoza la Ufufuo na Uzima lililoko Ubungo Dar es Salaam. "Wiki hii kuna jambo zito sana ambalo lilitokea kwenye Jimbo la Kawe, Rais wetu alikuwa anaelekea Bagamoyo, akapita Tegeta ambako mimi ni mfanyakazi wa wananchi kule. Wakati anaongea na wananchi, alisema ameamua kujitolea kutengeneza documentary ambayo itaitangaza Tanzania kwenye mataifa ya nje," alisema Askofu Gwajima.

"Unajua Tanzania ni nchi nzuri sana, lakini kule nje hatufahamiki sana, na kwa sababu ya kutokufahamika, kuna mambo mengi tunakosa, tuna vivutio vingi vizuri, 'investment' na maeneo mazuri sana ya utalii lakini huko nje hawajui. Sasa Rais ameamua yeye mwenyewe kwamba awe mdau wa kuitangaza Tanzania kwenye mataifa ya nje kwa kwenda sehemu mbalimbali kwenye vivutio ili Tanzania iwekwe kwenye ramani ya dunia, jambo hilo lilinigusa sana."

Askofu Gwajima alisema yeye ni miongoni mwa watu waliopata athari za kukutana na tatizo la Tanzania kutokujulikana katika nchi mbalimbali alikokuwa akienda kufundisha. "Kati ya watu waliopata athari kwa sababu ya Tanzania kutokujulikana ni mimi mmojawapo, nimetembea duniani kufundisha watu wengi, nakumbuka siku moja nilifanya mkutano Tokyo nchini Japan, shida niliyokumbana nayo ni kwamba kila ukitaja Tanzania na ukisema tuna vivutio vingi sana wanakuambia hebu tuonyeshe kwenye ramani," alisema.

"Kuna vitu vingine tunavikosa kwenye kujenga uchumi wa Tanzania kwa sababu nchi yetu haijawa halisi sana kwenye ramani ya dunia, kwa maana ya maliasili zetu, mila yetu, upole wetu, upendo wetu. Kwa hiyo kile kitendo cha Rais Samia kujitolea yeye mwenyewe kuanza kuimarket nchi yake ni jambo gumu sana kwa Rais ambaye ana majukumu mengi sana kwa sababu inagharimu muda, kuumia na hilo jambo limekuwa zuri sana."

"Kitendo kinachofanywa na Rais, tunatakiwa kukisapoti watu wote na tunatakiwa kumshukuru Mungu kwamba Rais amejitolea kufanya hiyo kazi na mwisho wa siku watalii watakuja, watu watapata fedha, watu watagundia 'investment' za Tanzania, vitu vilivyopo na matokeo yake uchumi wetu utaanza kwenda juu kwa sababu tumeanza kufahamika."

"Na kwa jambo hilo, Rais anatakiwa kupigiwa makofi makubwa kuliko tuliyowahi kumpigia na anatakiwa kutiwa moyo ili asonge mbele na kazi hiyo, kazi ni ngumu na sisi tunamsapoti asilimia 100."

Summons to appear(O.VR.20(1)of (CPC) (substitute service)

**IN THE RESIDENT MAGISTRATES COURT OF**
**DAR ES SALAAM AT KINONDONI**
**EXTENDED LAND APPEAL NO 2 OF 2021**
**MARSHA J.BUKUMBI…….APPEALANT**
**VERSUS**
**WILLIAM MUZE& OTHERS…….RESPONDENT**

**TO.**

**1.AUGUSTINO L MIKITO**
**2.MOSES ELISHA ILOMO**

**WHEREAS:** the above named **APPEALANT** has institute the appeal against you,you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized agent on 19th day of **OCTOBER 2021 at 09:00AM before Hon. A.CHUGULU SRM**,in the morning to answer the said Appeal and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your **REPLAY**

**TAKE NOTICE** that,in default of your appearance on that the said matter will be heard and determined in your absence.

Given under my hand and the seal of this court ,this **1st day of September, 2021**

HABARI KITAIFA

# Rukhsa kuchanganya chanjo za corona

## •Kwenye mikusanyiko tahadhari izingatiwe

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na UVIKO-19, serikali imesema inasimika mitambo 25 ya kutengeneza mitungi ya Oksijeni kupitia ufadhili wa Global Fund.

Vilevile, wataalamu wa afya wamebainisha kuwa inaruhusiwa kuchanganya chanjo za corona zilizoidhinishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), lakini kwa masharti ya kuzingatia muda wa kuchanjwa pamoja na kuwiana kiutendaji kati ya chanjo zinazochanganywa.

Katika semina ya kuelimisha wabunge kuhusu UVIKO-19 iliyofanyika bungeni jijini Dodoma jana, Mkurugenzi wa Huduma za Kinga wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, alisema ufungaji wa mitambo hiyo ya Oksijeni unaendelea kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Dk. Subi alisema mitambo hiyo itafungwa kwenye hospitali za halmshauri kwa lengo la kutatua kero ya upatikanaji wa Oksijeni pindi kunapokuwa na wagonjwa wengi.

"Tunachukua tahadhari, tusikimbilie Oksijeni bali tukimbilie kinga kwanza. Lakini hii ni vita lazima tujipange, fedha za Global Fund zinaendelea kutoka, mitambo inaendelea kufungwa.

"Kwa sasa tunafunga mitambo 25 kwenye hospitali za halmashauri kutokana na sapoti ya hizi fedha," alisema Dk. Subi wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum Halima Mdee (CHADEMA) aliyehoji mikakati ya serikali kuhakikisha mitungi ya Oksijeni inapatikana kwenye hospitali zote nchini.

Dk. Subi aliongeza kuwa mwanzoni kulikuwa na mitambo saba pekee nchini na kwamba fedha hizo za Global Fund hazitaishia wizarani bali zitashushwa hadi ngazi za chini kwenye kamati za afya za vijiji.

Alibainisha kuwa hadi kufikia juzi, watu 331,000 nchini walikuwa wamechanjwa chanjo ya kujikinga na ugonjwa huo.

**ZANZIBAR KUCHANJWA MARA MBILI**

Akifafanua kuhusu suala la wananchi wa Tanzania Zanzibar kuzuiwa kwenda kuhiji Macca licha ya kuchanja chanjo ya Cinovac na kutakiwa kuchanja ya Johnson&Johnson, Dk. Subi alisema suala hilo limewashangaza hata wao huko wizarani.

Alisisitiza wataalamu wao wanaendelea kushughulikia suala hilo kwa kuwa chanjo ya Cinovac ni miongoni mwa nane zilizoidhinishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kati ya chanjo zaidi ya 300 zilizotengenezwa kukabiliana na virusi vya corona.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, akichanjwa chanjo ya COVID -19. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**KUZUIA MIKUSANYIKO**

Akijibu swali la Mbunge wa Buchosa, Erick Shigongo (CCM), aliyehoji sababu za kuendelea kuwapo mikusanyiko na matamasha makubwa nchini licha ya serikali kupiga marufuku, Waziri wa Afya, Dk. Dorothy Gwajima, alisema serikali inalazimika kutumia busara kuruhusu kufanyika kwa makongamano hayo kutokana na mazingira halisi ya kiuchumi nchini.

"Ukizuia kabisa mikusanyiko itakuwa balaa kutokana na mazingira yetu ya kiuchumi, ndege tunapanda, tunakusanyika kwenye chai, muhimu ni kuzingatia 'social distance'.

"Sasa shida iliyopo watu wanakusanyika bila kuchukua tahadhari na unakuta kwenye mikusanyiko hiyo viongozi wapo na hawachukui hatua.

"Hatuwezi kuzuia kabisa mikusanyiko kutokana na mazingira yetu, busara lazima itumike, kuna mambo yatakwama kabisa kiuchumi tukichukua uamuzi huo," alifafanua.

Waziri Dorothy pia alitangaza kuongeza dau kutoka Sh. milioni moja aliyoahidi awali hadi Sh. milioni mbili kwa yeyote atayethibitisha kwamba serikali iliwahi kutangaza msimamo kuwa kamwe haitaruhusu chanjo yoyote ya corona kutolewa nchini.

Pia alisema atatoa Sh. 200,000 kwa mtu atakayetoa uthibitisho sahihi kuhusu suala hilo kwamba wakati wa uongozi wa awamu ya tano, serikali ilisema haitakimbilia kupokea chanjo hizo hadi itakapojiridhisha kwanza juu ya usalama wake kwa wananchi.

Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliwataka wabunge kushiriki kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kuchanja chanjo ya corona.

Kiongozi huyo wa Bunge alitoa angalizo kwamba kuna shida imeibuka ya watu waliochanja kuwaona wasiochanja kama maadui.

"Msiende na kwa wasiochanja wapeni fursa ili waone umuhimu wa kupata chanjo. Rais amesema chanjo ni hiari sisi tuliochanja tusiwahukumu wasiochanja, tusiwahukumu wanaopinga chanjo tuwape nafasi ya kuelimika," alihadharisha.

Naibu Spika alimwagiza Waziri mwenye dhamana kufuatilia hali ya upatikanaji wa mitungi ya Oksijeni ili maeneo yenye uhaba hatua zichukuliwe haraka kuokoa maisha ya wananchi.

**CHANJO KUZUIA MIMBA**

Kuhusu hoja kwamba chanjo hiyo inasababisha wanawake kutoshika ujauzito, Profesa Gerald Misinzo kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), alisema dhana hiyo ni potofu.

Prof. Misinzo ambaye ni mjumbe wa kamati iliyoundwa na Rais kuishauri serikali hatua za kuchukua dhidi ya UVIKO-19, alibainisha kuwa kati ya chanjo nane zilizoidhinishwa na WHO, Johnson & Johnson ni 'baba lao' kwa sababu inaweza kuhifadhiwa hata kwa jokofu la kawaida na pia mtu anachomwa mara moja tu.

**KUCHANGANYA CHANJO**

Mtaalamu huyo alisema inaruhusiwa kuchanganya chanjo hizo, lakini lazima kuwa na tahadhari kwa kuhakikisha unatumia chanjo zenye sifa zinazowiana.

Alifafanua kuwa mtu anayehitaji kuchanganya chanjo za corona pia atatakiwa baada ya kupewa chanjo ya kwanza, ahakikishe zinapita siku 28, yaani wiki nne kabla ya kupewa chanjo nyingine.

**WAJIBU WA WABUNGE**

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichwale, alisema wabunge wanapaswa kufahamisha wananchi kuzingatia afua za chanjo dhidi ya ugonjwa huo.

Vilevile, alisema wanasiasa hao pia wanatakiwa kusaidia kutoa taarifa sahihi kuhusu shida za kiutendaji zinazoibuka, kushiriki kutoa elimu ya corona kwa wananchi na kutoa misaada katika kuwezesha elimu hiyo kwa wananchi.

Stanslaus Nyongo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Maendeleo ya Jamii, aliyekuwa anaongoza semina hiyo, aliishukuru Wizara ya Afya kwa kuandaa semina hiyo kwa wabunge.

Alibainisha kuwa hiyo ilikuwa mara ya pili kwa watunga sheria hao kupewa mafunzo kuhusu UVIKO-19 wakiwa bungeni, mara ya kwanza wakielimishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. Mohamed Janab.

# Bil 7.8/- kuboresha huduma za Posta

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imesema imewekeza Sh. bilioni 3.9 kati ya Sh. bilioni 7.8 ilizoahidi kulipatia Shirika la Posta, zitumike kuleta mabadiliko ya kidijitali pamoja na kufanya ununuzi wa vitendea kazi vya usafirishaji.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Faustine Ndugulile, alisema hayo wakati alipokagua maandalizi ya uzinduzi wa 'Huduma Pamoja' unaotarajiwa kufanyika leo katika makao makuu ya shirika hilo jijini Dar es Salaam.

Katika ukaguzi huo Dk. Ndugulile alisema mikakati ya serikali kwa sasa ni kulifanya shirika hilo kuwa kitovu cha biashara mtandao na juhudi za kulifanikisha hilo bado zinaendelea.

"Ukuaji wa teknolojia unaoendelea kufanyika ndani ya shirika hili kwa kuainisha huduma mbalimbali za kidijitali ikiwamo duka mtandao la Posta (Posta Online shop) pamoja na Posta kiganjani, na niahidi serikali italinda watumiaji wa mtandao na kupambana na matapeli wa mitandaoni ili kurahisisha ukuaji wa biashara hizi nchini," alisema Ndugulile.

Vile vile, alisema mradi wa Dola milioni 150 za Kimarekani zitatumika kwenye vituo vya huduma pamoja nchini.

Tanzania pia imepata ushindi kwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Utawala na Baraza la Uendeshaji la Umoja wa Posta duniani ambao ulainisha faida zitakazopatikana kwa ushindi huo ikiwamo ya taifa kupata nafasi ya kuwa sehemu ya watoa maamuzi ya mambo mbalimbali yanaogusa moja kwa moja sekta ya Posta nchini, Afrika kwa ujumla na ndani ya umoja huo katika ngazi ya dunia.

Kwa upande wake Kaimu Postamasta Mkuu wa shirika hilo, Macrice Mbodo, alieleza namna ya kujisajili na duka mtandao na faida ambazo shirika pamoja na mteja atapata katika duka hilo.

"Mfanyabiashara anapojiunga katika huduma ya duka mtandao na kuuza bidhaa zake sisi kama shirika tunapata asilimia tatu ya bei ya bidhaa sambamba na gharama za usafirishaji na hilo limesaidia shirika kupata Sh. milioni 300 toka kuzinduliwa kwa huduma ya duka mtandao," alisema Mbodo.

Alisema mwelekeo wa shirika hilo katika kuziweka huduma zake zote kiganjani namba ya simu ya mteja itakuwa anwani yake, pia katika awamu ya kwanza kutakuwa na vituo 10 vya Huduma Pamoja kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Arusha, Kigoma, Mbeya, Tanga, Morogoro, Kigoma, Mjini Magaribi-Unguja na Chakechake Pemba.

Pia awamu ya pili itakuwa na mikoa 17 ili kuiwezesha kufikisha huduma hiyo nchi nzima, na shirika hilo linazindua rasmi huduma ambayo itazikutanisha taasisi mbalimbali za serikali na kutoa huduma kwa pamoja i kiwemo BRELA, NIDA, NSSF, RITA, TRA Uhamiaji, PSSF, NHIF ambazo zitatoa huduma kwa pamoja kupitia ofisi za Posta nchini.



Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe mkoani Geita, Charles Mbeho, akiwahutubia wachimbaji wadogo katika kijiji cha Nyambogo, ambapo Waziri wa Madini, Doto Biteko alifanya ziara ya siku moja baada ya gazeti la Nipashe kutoa taarifa ya mchimbaji mdogo aliyekuwa akichimba choo nyumbani kwake na kupata mawe ambayo yanasadikiwa kuwa ni madini ya dhahabu wiki moja iliyopita. **PICHA: MOHAB DOMINICK, GEITA**

# Mkumbo aanika faida za AfCFTA kwa Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, amesema Tanzania itapata faida nyingi za kiuchumi endapo itaridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA).

Aliyasema hayo wakati akijumuisha maoni na mapendekezo kwenye semina iliyolenga kuwaelimisha wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Alisema serikali imeshafanya uchambuzi wa faida na hasara za mkataba huo na kujiridhisha kuwa faida ni kubwa kuliko hasara iwapo Tanzania itaridhia kujiunga na mkataba huo.

Akitaja faida hizo, Prof. Mkumbo alitaja faida hizo kuwa ni pamoja na kupatikana kwa masoko mapya ya mazao ya kilimo na hivyo kuchochea uzalishaji wake nchini.

Faida nyingine zilizotajwa ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji na ajira kwa wakulima na wadau wanahusisha katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo, upatikanaji wa bidhaa za aina mbalimbali nchini na kupatikana kwa soko kubwa la bidhaa na huduma lenye idadi ya watu takribani bilioni 1.2 ukilinganisha na idadi ya watu milioni 522 katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Prof. Mkumbo alisema faida zingine ni kuongezeka kwa tija na ubora kwa bidhaa na huduma za Tanzania kutokana na kuongeza kwa ushindani.

Faida nyingine ni unaruhusu kutoridhia kwenye baadhi ya maeneo ambayo nchi itaona haina faida.

Alisema mkataba huo pia umetambua utofauti wa uchumi katika nchi za Afrika, kuweka namna ya kuzisaidia nchi ambazo uchumi wake siyo mzuri huku ikitoa fursa ya kujindoa baada ya miaka mitano.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Mtangamano wa Biashara wa Wizara, Ally Gugu, alisema mkataba huo unahusisha maeneo ya ushirikiano katika itifaki ya biashara ya bidhaa, huduma, usuluhishi wa migogoro, uwekezaji, haki miliki ubunifu, sera za ushindani, na biashara mtandao.

Alisema kuridhia mkataba huu kutaongeza wigo wa fursa nafuu za biashara na masoko ya biashara, kutoa soko la uhakika na bila kutengeneza masoko ya upendeleo na fursa zaidi ya ushindani na fursa za biashara.

## Jela miaka 30 kubaka mhudumu wa baa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imemhukumu mkazi wa Katoro, Justini Silivini (24), kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kwa kosa la kubaka.

Alitiwa hatiani na kupewa adhabu hiyo baada ya mahakama hiyo kuridhika kuwa alimbaka mwanamke mwenye umri wa miaka 21 na kumsababishia maumivu.

Hukumu hiyo ilitolewa Ijumaa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samuel Maweda, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo paspo kuacha shaka yoyote.

Hakimu Maweda alisema Mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili liwe fundisho kwake na kwa vijana wengine wenye tabia ya kikatili kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mahakamani shahidi mmoja, ambaye alithibitisha kuwa alibakwa na mshtakiwa huyo.

Aidha, Hakimu Maweda alisema mshtakiwa huyo alikwenda kwenye baa iliyopo Mtaa wa Afya Katoro, ambapo mlalamikaji (jina lake limehifadhiwa) anapofanyia kazi.

Alisema baada ya mshtakiwa kufika kwenye hiyo baa alimkuta mlalamikaji akiwa anafanya kazi zake, ndipo mshtakiwa huyo alimshika mkono na kumvuta kwa nguvu, huku akiwa na kisu mkononi hadi pembeni mwa baa hiyo na kumvua nguo na kuanza kumbaka.

Aidha, alisema mlalamikaji huyo alipiga kelele ndipo wasamaria wema walifika na kumkamata mshtakiwa huyo na kumpeleka katika Kituo cha Polisi Katoro na baada ya mahojiano mshtakiwa alipelekwa katika Mahakama ya Wilaya Geita.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Clemence Kat, alidai mahakamani kuwa Oktoba 20, mwaka 2020 maeneo ya Katoro Mkoa wa Geita, mshtakiwa alimbaka mwanamke mwenye umri wa miaka 21 na kumsababishia maumivu makali sehemu zake za siri.

## Madiwani watakiwa lengo makusanyo

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MKURUGENZI mpya wa Halmashauri ya Gairo, Asajile Mwambambale, amewataka madiwani wa halmashauri kufikia lengo la makusanyo ya zaidi ya Shilingi bilioni moja kwa mwaka wa fedha 2021/ 2022.

Mwambambale alitoa rai hiyo katika kikao cha Baraza la Madiwadi la halmashauri hiyo na kubainisha lengo la ukusanyaji wa kodi ni kusaidia shughuli za maendeleo ikiwamo umaliziaji wa majengo ya shule na zahanati zilizoanza kujengwa kwa nguvu ya wananchi.

Alisema ukusanyaji kodi unatakiwa kumgusa kila mwananchi anayepaswa kulipa bila kumwonea mtu ikiwa ni katika azma ya kupandisha makusanyo ya ndani na kuondokana na dhana ya wilaya hiyo kuwa ya mwisho katika ukusanyaji.

"Pamoja na mambo mengine kazi kubwa kwangu kama mkurugenzi ni kuhakikisha ukusanyaji mapato unaongezeka katika halmashauri, niwaombe tushirikiane kukusanya kodi bila kumwonea mtu, lakini tusiogope malalamiko ya baadhi ya watu kwa sababu ni ukweli hawajazoea kulipa," alisema.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Rechal Nyangasi, alisema dhamira ya serikali kuongeza ukusanyaji wa mapato katika halmashauri ni hatua nzuri ambayo itawasaidia wananchi kupata maendeleo kwa haraka.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Taifa Stars malizeni biashara mapema kwa Mkapa kesho

**KWA** mara nyingine tena timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, itashuka dimbani kesho, baada ya kutoka sare bao 1-1 ugenini dhidi ya DR Congo kwenye mechi yao ya kwanza ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar.

Kwa matokeo hayo, Stars sasa ina alama moja sawa na DR Congo huku Benin ikiwa kileleni katika Kundi J, baada ya Ijumaa iliyopita yenyewe kuibuka na ushindi wa bao 1-0 ugenini dhidi ya Madagascar.

Hivyo, Stars ambayo itaikaribisha Madagascar katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho, ushindi pekee ndio utakaohitajika kwake ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kumaliza nafasi ya kwanza kwenye Kundi lao la J.

Ikumbukwe katika mbio hizo za kuwania kufuzu Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar, kwa Ukanda wa Afrika kuna makundi 10, na kila timu itakayomaliza nafasi ya kwanza kwenye kundi lake ndiyo itakayotinga hatua inayofuata ya kuwania tiketi tano za kushiriki fainali hizo.

Kwa Ukanda wa Afrika unatakiwa kutoa wawakilishi watano tu kushiriki fainali hizo, hivyo baada ya kupatikana timu 10 zitakazoongoza makundi yao, kutachezwa tena mechi za mchujo ili kupata miamba mitano itakayotinga Qatar mwakani.

Kwa mantiki hiyo, Stars inatakiwa kupigana kiume katika mchezo huo wa kesho huku ikihakikisha haipoteza mechi yoyote hususan inapokuwa uwanja wake wa nyumbani na kisha ugenini kwenda kusaka matokeo chanya ama angalau sare, lakini si kukubali kupoteza.

Tunaamini kwa soka lililoonyesha Ijumaa tena ikiwa ugenini nchini DR Congo, Stars ina nafasi kubwa ya kupata matokeo chanya kesho kama wachezaji watajituma zaidi na kuona thamani ya kuvaa jezi ya taifa kwa niaba ya Watanzania zaidi ya milioni 50.

Aidha, Nipashe tunatambua mashabiki ni mchezaji wa 12 uwanjani hususan timu inapokuwa uwanja wake wa nyumbani, hivyo kila mmoja kwa nafasi yake kesho iwe siku ya kujitokeza kwa wingi Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenda kuipa sapoti Stars katika mchezo huo ambao ni wazi utakuwa mgumu kwa kila upande.

Matarajio yetu si kuona idadi kubwa ya mashabiki wakijitokeza kwa wingi uwanjani pekee, bali pia kuwashuhudia wakibeba jukumu lao la kushangilia mwanzo mwisho katika mchezo huo, ambao kama Stars ikishinda inaweza kuwa miongoni mwa timu zitakazokuwa katika nafasi nzuri ya kuongoza kundi lao.

Tunatambua matokeo chanya pekee kwa Benin, ndiyo yanayoweza kuizuia Stars kukaa kileleni endapo tu itashinda kesho, kwani kama Wabenin hao watapoteza, DR Congo itakuwa na pointi sawa na Tanzania ikishinda, lakini endapo Wakongomani hao watapoteza basi Benin itaendelea kuongoza kundi hilo.

Hivyo, biashara kwa Stars inapaswa kuwa mapema kwa kutafuta matokeo kwenye mechi hizi za awali, na haipaswi kujisuasua hadi kusubiri matokeo ya mechi za raundi ya mwisho kuanza kupiga hesabu za kuombea timu nyingine kupoteza katika kundi lake ili kupata nafasi ya kusonga mbele.

Ingawa tunatambua hautakuwa mchezo rahisi kwa Stars hasa ukizingatia Madagascar ilipoteza mchezo wa awali, hivyo itataka angalau kupata pointi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele, lakini dhamira, kujitoa na kuthamini jezi ya taifa kwa wachezaji wakiungwa mkono na mashabiki kuishangilia mwanzo mwisho, hakuna litakaloshindikana kesho kwa Mkapa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Usajili 2021/22 uende sambamba na ubora wa viwanja, waamuzi

Na Adam Fungamwango

**MASHABIKI** wa soka nchini kwa sasa wameonekana kuchoshwa na tambo za nje ya uwanja, ambazo wakati mwingine hazina kichwa wala miguu, hivyo wanaisubiria kwa hamu kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Uwanjani ndiyo mwisho wa kila kitu. Unaweza kutamba huku na kule, lakini mwisho wa siku kama timu haina kitu uwanjani, hata yale ya nje ya uwanja yanakuwa hayana maana tena. Mashabiki wengi wanaombea hata leo ligi ianze ili waangalie mambo mbalimbali ambayo wanayaona na kuaminishwa.

Kwanza kabisa udhamini mnono wa Kampuni ya Azam, unadhaniwa utafanya timu nyingi kutokuwa na matatizo ya kifedha.

Kutokuwa na matatizo ya kifedha kunadhaniwa na mashabiki wengi kuwa timu zitakuwa imara, hivyo kutoa ushindani mkubwa na kuepuka tabia ya baadhi ya timu au wachezaji 'kuuza mechi' kwa kucheza chini ya kiwango, baada ya kuhongwa.

Udhamini huo unategemewa kuwa klabu zitasajili wachezaji wazuri, wenye uwezo wa hali ya juu wa kupambana kuifanya ligi kuwa ngumu, zenye mechi zisizotabirika. Hii imeonekana kwenye usajili. Ukiangalia klabu nyingi msimu huu zimejitahidi mno kwenye kusajili wachezaji bora na wenye uwezo.

Klabu kama Mtibwa Sugar na Kagera Sugar ambazo kwa utamaduni wao zilikuwa hazisajili wachezaji wa kigeni, lakini safari hii zimefanya hivyo.

Kupungua kwa timu kutoka 18, hadi 16, pia kunaonekana kuifanya Ligi Kuu msimu wa 2021/22 kuwa ngumu na isiyotabirika. Timu zote zitacheza mechi 30 tu ili kupata bingwa.

Kushuka kwa Ihefu FC na Gwambina FC, huku wachezaji wake bora wakienda kuongeza nguvu kwenye klabu zilizobaki Ligi Kuu, nako pia kunaelezwa kuwafanya mashabiki wengi kuwa na hamu ya kutaka kuona itakuwa ni ligi ya aina gani.

Mpaka hapo utaona jinsi klabu mbalimbali zilivyojiandaa kisawasawa na ligi. Lakini kuna jambo moja ambalo kama halitofanyika, ule msisimko, ladha na hamu ya mashabiki haitoweza kufikia.

Ni upande wa uwanja na waamuzi, wala si siri, kuwa viwanja vingi vya Tanzania bado ni tatizo kubwa. Hata serikali inaelewa hilo, ndiyo maana imeondoa kodi ya nyasi bandia.

Shirikisho la Soka nchini (TFF), Bodi ya Ligi, kwa kushirikiana na wamiliki wa viwanja, wanatakiwa waviboreshe ili mashabiki wafurahie ufundi wa wachezaji kwenye kusakata kandanda na kuonyesha ufundi wao, badala ya kuangalia butuabutua.

Haiwezekani klabu zisajili wachezaji bora, halafu watatizwe na uwapo wa viwanja vibovu. Kuna kamati ya kukagua viwanja ambayo inapita viwanja vyote kwa ajili ya kuvipitisha.

Hata hivyo, kitu ambacho TFF imeshindwa kujua ni kuwa kuna wakati viwanja vinakuwa bora hususan mwanzo wa ligi, lakini baada ya kuchezewa mechi kadhaa, vinakuwa vibovu kuliko kawaida. Lakini kwa sababu tayari vilishapitishwa, bado vinaendelea kutumika.

Sehemu nyingine ni waamuzi. Waamuzi nao wamekuwa ni sehemu ya tatizo kwenye soka la Tanzania, hasa katika baadhi ya maamuzi yao.

Ingawa msimu uliopita waamuzi kwa kiasi kikubwa walijitahidi kupunguza makosa mengi ambayo yalionekana misimu kadhaa nyuma, lakini wanatakiwa kupunguza zaidi kuelekea msimu mpya wa ligi kwa sababu klabu zimetumia gharama kubwa kusajili na kuandaa timu.

Kinachotakiwa ni timu iliyojipanga vizuri siku hiyo, ishinde mechi na si kutafuta namna ya kuisaidia timu iliyoshindwa mbinu. Ni dhambi kubwa timu iliyokuwa kwenye kiwango cha hali ya juu siku ya mechi, ikanyimwa ushindi kwa sababu ya uamuzi mbovu.

Siyo ajabu mwamuzi kufanya makosa, hii inatokea hata kwa waamuzi Ulaya, lakini wakati mwingine kwa waamuzi wa Bongo inazidi kutokana na mapenzi na mahaba kwa waamuzi na klabu mojawapo ama maslahi binafsi.

Kwa mechi moja, mwamuzi anaweza kufanya makosa zaidi ya sita. Halafu kwa hali ya kushangaza unaweza kukuta yote yanaiumiza timu moja tu. Chama cha Waamuzi Tanzania (FRAT), na Kamati ya Waamuzi kwa sasa wafanye kazi ya kuwanoa waamuzi wao ili watende haki kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Pia, nadhani umefika wakati Tanzania kuanza kufikiria kutumia VAR, kwa baadhi ya mechi, kama siyo zote ili kuwasaidia waamuzi wetu, lakini pia kupunguza ama kuondoa lawama kwa waamuzi kutoka kwa baadhi ya viongozi wa klabu na mashabiki wa soka nchini.

HABARI KITAIFA

## Wenye mashine za mbao wapata fursa mikopo nafuu

**Na Mwandishi Wetu,** MAFINGA

BENKI ya Biashara Tanzania (TCB) kwa kushirikiana na Taasisi ya Maendeleo ya Misitu Nchini (FDT) na Kampuni ya LonAgro Tanzania wameingia makubaliano ya kutoa mikopo nafuu ya mashine za kuchana mbao.

Lengo la mikopo ni kuongeza uzalishaji wa mbao zenye ubora zaidi zitakazoweza kuingia kwenye ushindani katika soko la ndani na nje ya nchi.

Mkurugenzi wa Mikopo wa TCB, Henry Bwogi, alisema mikopo hiyo inakusudia kukuza sekta ya misitu ili kuchangia zaidi katika pato la taifa na kuinua hali ya uchumi wa wananchi.

"Kumekuwa na changamoto kubwa katika upatikanaji wa mashine bora za kuchana mbao, hivyo tumetumia fursa hii kuongeza nguvu ili sekta ya misitu iweze kufanya vizuri na kuongeza mapato ya serikali sambamba na kuinua maisha ya mtu mmoja mmoja," alisema Bwogi.

Alieleza kuwa makubaliano hayo yenye masharti nafuu yamewalenga wafanyabiashara na wajasiriamali katika sekta ya misitu hivyo ni wao kuchangamkia fursa hiyo ili kuzalisha bidhaa bora zitakazokuwa na ushindani wa bei sokoni.

Alisema kumekuwa na matumizi ya teknolojia duni katika sekta ya misitu inayopelekea hasara kwa wafanyabiashara hivyo kupitia mikopo hii itawawezesha kupata mashine bora za kisasa ambazo zitawasaidia kuongeza uzalishaji wa mbao.

Rais wa Shirikisho la Viwanda vya Misitu Tanzania, Ben Mfungo Sulus, aliishukuru Benki ya TCB na FDT kwa kuleta mradi huo katika Wilaya ya Mufindi na kusema atawahamasisha wafanyabiashara katika sekta ya misitu kuchangamkia fursa hiyo ili kujipatia mashine zitakosaidia kurahisisha kazi na kuongeza ubora na thamani ya

## TGNP yataka elimu mitandao ya kijamii

**Na Yasmine Protace**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP) umetaka jamii ipatiwe elimu juu ya mitandao ya kijamii, ili mitandao hiyo isitumike kwa kuwadhalilisha wanawake kijinsia.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, katika mada iliyozungumzia matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii katika kuchochea usawa wa kijinsia.

Mada hiyo iliyotolewa katika Semina za Jinsia na Maendeleo (GDSS), ambapo Liundi alisema ili kukomesha matukio ya ukatili katika mitandao ya kijamii, inatakiwa elimu itolewe kwa jamii.

"Mitandao ya kijamii ni maisha ya taswira, kama hakutakuwa na elimu ya kutosha kwa jamii, suala la matumizi mabaya ya mitandao litazidi kuendelea," alisema.

Alisema baadhi ya watu wamekuwa wakitumia mitandao hiyo kuwadhalilisha wanawake.




Meneja Mradi wa Magomeni Kota kutoka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Bernard Mayemba (kulia), akitoa maelezo kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho (katikati), aliyeongozana na maofisa wa wizara hiyo, kuhusu hatua ya mradi huo juzi, ambao umekamilika kwa asilimia 99 na wakazi kutarajia kuhamia Oktoba, mwaka huu. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

## Mahitaji maji Simiyu yazidiwa kiwango

**Na Happy Severine,** BARIADI

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu (BARUWASA), imesema mahitaji ya maji katika eneo hilo ni makubwa ikilinganishwa na uzalishaji wanaofanya kila siku.

Meneja wa BARUWASA, Musalila Masatu, alisema hayo katika mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, uliofanyika eneo la stendi ya zamani mjini Bariadi.

Kabla ya meneja huyo kueleza hayo katika katika mkutano huo, wananchi walilalamika kwa mkuu huyo wa mkoa kutopatikana huduma ya maji katika maeneo yao kwa zaidi ya siku tatu hadi nne.

Mmoja wa wananchi hao, Mariamu Majiku, alisema huduma ya maji imekuwa kero kwa kuwa katika mtaa wa Sima anapoishi wanapata maji mara moja kwa wiki.

Kafulila alimtaka meneja huyo kutoa ufafanua na kueleza kwamba BARUWASA, kiwango cha maji kinachozalishwa ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji ya wananchi. Masatu alisema mahitaji ya wakazi wa mji huo kwa siku ni lita milioni saba na mamlaka hiyo uwezo wake kwa sasa ni kuzalisha lita milioni mbili sawa na asilimia 35 ya mahitaji.

"Mamlaka vyanzo vyake vya maji ni visima virefu ambavyo ni zaidi ya 20, lakini visima hivi ukifika wakati wa kiangazi kama sasa vinapungua maji, hivyo uhitaji unakuwa mkubwa kuliko uzalishaji," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo mamlaka inatoa maji kwa mgao ili kuwahudumia wananchi wote.

Katika mkutano huo Kafulila alipiga marufuku magari madogo (mchomoko) kuingia mjini kuchukua au kushusha abiria na badala yake waishie stendi kuu ya magari yote makubwa na madogo Somanda.

Alisema kuwa serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 18 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara za mjini na vijijini zilizoko chini ya TARURA na kuwataka wataalamu kusimamia fedha hizo kwa uadilifu.

## ACT-Wazalendo yaweka msimamo tozo miamala

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kinaendelea kusimamia kauli yake ya kupinga uamuzi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweka tozo katika miamala ya simu, kwa madai kuwa hatua hiyo inazidisha ukali wa maisha.

Katibu wa Habari, Uenezi, Mawasiliano na Umma wa chama hicho upande wa Zanzibar, Salum Bimani, alisema chama hicho kinazitaka serikali kuacha kubuni mipango ya kuwaathiri na kuwakandamiza wananchi kimapato na kimaisha pamoja na kuzitaka ziachane na sera mbovu zinazosababisha kuwadhoofisha kiuchumi wananchi maskini wanaohangaika kujinasua kimaisha.

Kwa mujibu wa taarifa yake aliyoitoa jana kwa vyombo vya habari, Bimani alisema ACT-Wazalendo pia kinahoji uamuzi wa fedha hizo kuelekezwa Tanzania Bara pekee wakati biashara ya miamala ya fedha ya kitaifa na kimataifa inatumika katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano.

"Ni dhahiri kwamba Wazanzibari walio wengi ni watumiaji wakubwa wa mitandao yote ya simu iliyopo Tanzania, ikiwamo ya TTCL, Zantel, Vodacom, Airtel, Tigo na Halotel. Serikali ya Jamhuri ya Muungano imetangaza kwamba kwa mwezi mmoja na nusu tokea tozo hizo zianze kukusanywa, jumla ya Shilingi bilioni 63 zimekusanywa," alisema.

Alitaka serikali kuujulisha umma ni kiasi gani cha fedha hizo kimewasilishwa Zanzibar ili kutekeleza miradi ya kujenga madarasa na vituo vya afya kama iliyokusudiwa kwa sababu Wazanzibari wana haki ya kujua makato ya tozo kutokana na miamala inayofanywa ndani ya Zanzibar au kutoka na kuingia Zanzibar yanawafaidisha vipi.

"ACT-Wazalendo kinashangazwa sana kwamba hadi sasa serikali zote, ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zimekaa kimya juu ya jambo hilo".

Vile vile, aliwataka wananchi wazidi kuwa makini na wasichoke kuwaunga mkono katika kupaza sauti kila inapojiri maamuzi ya mamlaka au sera zisizofaa, ambazo zinalenga kuwanufaisha wachache.

# Tani 16,000 mahindi zadaiwa kukosa soko

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

TANI 16,000 za mahindi wilayani Ludewa mkoani Njombe, zinadaiwa kukosa soko endapo ununuzi wa mahindi na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) utafungwa baada ya kununua tani 1,000 pekee.

Hayo yamebainishwa na Mbunge wa Jimbo la Ludewa, Joseph Kamonga, baada ya kutembelea kituo cha ununuzi wa mahindi kilichoko kijiji cha Mlangali na kupokea kero mbalimbali kutoka kwa wakulima waliofika na kuuza mazao yao.

"Ukiacha chakula, tuna tani za ziada 17,000 za mahindi, lakini NFRA wamenunua tani 1,000 pekee kwa hiyo tani 16,000 zinakosa soko," alisema Kamonga.

Alisema nia kubwa ya kutembelea kituo hicho ni kutokana na malalamiko mengi aliyokuwa akiyapokea kutoka kwa wananchi wakati akiwa jijini Dodoma.

"Nia yangu ya kuja hapa ni kutokana na malalamiko mengi ambayo nikiwa bungeni Dodoma nilikuwa nikiyapokea kila siku mpaka hapakaliki. Kwenye bei pia mahindi yananunuliwa shilingi 430 kwa kilo, mwanzoni wananchi walishangilia waliposikia yanauzwa 500 kwa kilo, lakini baadaye yakaanza mabadiliko ya bei hii imeleta malalamiko sana kwa wakulima na wanahofu hapa katikati imebadilisha kumbe toka mwanzo wangekuwa wametoa bei elekezi kwa kila eneo hii ingepunguza malalamiko," alisema Kamonga.

Alisema wananchi wakulima wamekuwa na kero ya kusafiri umbali mrefu wengine kilomita 78 kufuata kituo cha ununuzi wa mahindi kilichopo kijiji cha Mlangali huku awali katika wilaya hiyo kulikuwa na vituo vitatu.

"Kwa miaka mingi Ludewa kumekuwa na vituo vitatu, kituo cha Ludewa vijijini, Mlangali pamoja na kituo cha Shaurimoyo na hii imekuwa ikiwarahisishia wakulima kufikisha mazao kwenye soko kirahisi, lakini kwa sasa tumewaongezea mzigo mkubwa sana wakulima," aliongeza Kamonga.

Alisema wananchi wana imani kubwa na ununuzi wa mahindi unaofanywa na NFRA huku akiahidi kushughulikia kero zilizojitokeza ili kuwasaidia wakulima wa Jimbo la Ludewa.




Meneja Mradi wa Magomeni Kota kutoka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Bernard Mayemba (kulia), akitoa maelezo kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho (katikati), aliyeongozana na maofisa wa wizara hiyo, kuhusu hatua ya mradi huo juzi, ambao umekamilika kwa asilimia 99 na wakazi kutarajia kuhamia Oktoba, mwaka huu. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Wafanyabiashara watelekeza soko

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BAADHI ya wafanyabiashara wilayani Shinyanga wametelekeza Soko la Didia ambalo lilijengwa na serikali kwa gharama ya Sh. milioni 107 kwa madai ya kukosa wateja na kuamua kuuza bidhaa zao sehemu zisizo rasmi.

Mtendaji wa kijiji cha Didia wilayani Shinyanga, Masano Kwiyela, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko alipotembelea soko hilo.

Kwiyela akizungumza kwa niaba ya Mtendaji wa Kata, alisema soko hilo lilijengwa mwaka 2012, lakini wafanyabiashara wamegoma kulitumia, wakidai kukosa wateja na kuamua kurudi mitaani kuuza bidhaa zao.

"Mkuu wa Wilaya, tunakuomba utusaidie wafanyabiashara waje walitumie soko hili kwa sababu serikali imetumia kiasi kikubwa cha fedha, lakini soko mpaka sasa halifanyi kazi na huduma zote zipo kikiwamo choo," alisema Kwiyela.

"Awali tuliwapa wafanyabiashara vibanda bure ili wafanye biashara zao, lakini muda mchache tu wakakimbia wote na soko kubaki tupu, wakidai hakuna wateja," aliongeza.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya, aliahidi kulifufua soko hilo kwa kuwaleta wafanyabiashara pamoja na kukarabati miundombinu ya barabara ili wateja wafike eneo hilo kwa urahisi.

Pia, aliahidi kuwaondoa wafanyabiashara wa gulio ambao wanafanya shughuli zao kwenye eneo la reli ili wakae jirani na soko hilo.

Alisema bado kuna eneo kubwa hekari 10 sehemu ambayo ni salama kwao na kuchangamsha soko hilo.

Baadhi ya wafanyabiashara walisema, wameshindwa kufanya biashara kwenye soko hilo kutokana na umbali hatua ambayo imesababisha wanunuzi kushindwa kufika.

# Utendaji kiwanda karatasi Mufindi ulivyomvutia RC

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, amevutiwa na utendaji kazi wa kiwanda cha Mufindi Paper Mills Ltd (MPM) cha Mgololo.

Akizungumza juzi wakati wa ziara ya kiwanda hicho, Sendiga alisema, ametembelea na kuona kazi nzuri inayofanyika na kuwa jitihada kubwa zinazofanyika kiwandani hapo ni faraja kwa sekta ya viwanda.

Alisema kiwanda cha MPM ni miongoni mwa bora vinavyofanya kazi yake kwa kuzingatia usalama wa wafanyakazi wawapo kazini kwa kuhakikisha wanakuwa na vifaa vya kazi kulinda usalama wao.

"Suala la usalama wa mazingira ya kazi kwa wafanyakazi ni jambo la msingi sana na nilipofika hapa kutembelea kiwanda hiki mbali ya kutazama mambo mengine ya uendeshaji, suala la usalama wa wafanyakazi nimelitazama na nimefurahishwa lilivyowekewa kipaumbele," alisema.

Pia aliagiza viwanda vingine ndani ya Wilaya ya Mufindi kuiga mfano wa MPM kwa kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi.

Kuhusu kiwanda kuendelea kudumisha uhusiano mwema na wananchi kwa kusaidia miradi mbalimbali ya kimaendeleo ikiwamo ya afya, alisema uwapo wa wawekezaji katika maeneo mbalimbali lazima suala la uhusiano mwema na wananchi wanaozunguka wawekezaji kuboreshwa na kuwa kinachofanywa na MPM katika kuendelea kujenga uhusiano mwema na jamii ni jambo zuri na la kupongezwa.

Kwa upande wake, Meneja wa kiwanda hicho, Mhandisi Gregory Chogo, alisema ziara hiyo ya Mkuu wa Mkoa imeshuhudia utendaji kazi wake.

Hata hivyo, alisema mwaka 2006 kulikuwa na mgomo katika kiwanda hicho na kusababisha wafanyakazi 660 kufukuzwa kutokana na mgomo na waliofukuzwa waliokuwa wakidai haki zao.

Mwaka 2018 kampuni ya MPM iliwalipa Sh. bilioni tano wafanyakazi hao na kumalizana nao, lakini walifungua kesi nyingine mahakamani kuidai serikali kuwalipa mkono wa kwaheri kwa kuachishwa kutoka SPM kuja MPM.

Akizungumzia uzalishaji kiwandani hapo, alisema hali ya uzalishaji ni nzuri na sasa wana oda za kutosha za bidhaa za karatasi, lakini kwa mwaka jana kutokana na janga la corona, uzalishaji

HABARI KITAIFA

# Lukuvi sasa ataka maonyesho ya kimataifa teknolojia, vifaa ujenzi

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameitaka Taasisi ya Shelter Afrique kuratibu maonyesho ya kimataifa ya dunia ya teknolojia na ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu nchini. Waziri Lukuvi alitoa kauli hiyo alipokutana na ujumbe wa taasisi hiyo katika ofisi za wizara eneo la Mtumba jijini Dodoma uliokwenda kwa ajili ya kuelezea mikakati yake kwa ajili ya kutangaza mikakati yake katika kusaidia ujenzi na teknolojia rahisi ya ujenzi kwa nchi wanachama.

Lukuvi alisema, serikali iko tayari kutoa eneo kwa ajili ya kufanyika maonyesho hayo kwa kushirikisha makampuni mbalimbali duniani aliyoyaeleza kuwa yataisaidia kutangazwa kwa teknolojia za ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu na hivyo kusaidia wananchi na kampuni zinazofanya kazi za ujenzi.

"Tunataka Shelter Afrique mratibu maonyesho na wadau wengine duniani kwa ajili ya kuonyesha teknolojia mpya au teknolojia nyingine kwa ajili ya ujenzi wa nyumba bora na gharama nafuu na maonesho hayo yawe ya kidunia" alisema Lukuvi.

Shelter Afrique ni taasisi ya kifedha yenye nchi wanachama 44 barani Afrika inayosaidia maendeleo ya ujenzi kwenye sekta ya nyumba na maendeleo ya mijini nchini Afrika ambapo hutoa bidhaa na mikopo ya fedha kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa nyumba bora za makazi kwa gharama nafuu.

Alisema, serikali iko tayari kutoa eneo la ekari 50 kwa ajili ya kufanyika maonyesho hayo kila mwaka kubainisha kuwa maonesho hayo yahusishe teknolojia rahisi ya ujenzi wa nyumba bora na vifaa vya ujenzi kwa lengo la kutoa elimu kwa makampuni ya ujenzi na wananchi kuweza kumudu gharama za ujenzi.

Kwa Tanzania, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) limekuwa katika jitihada kubwa za kujenga nyumba za gharama nafuu kwa ajili ya kuuza na kupangisha ambapo kwa sasa Shirika hilo linaendesha miradi yake maeneo ya Iyumbu na Chamwino mkoani Dodoma.

"NHC kwa sasa ina kiwanda cha kutengeneza matofali, eneo kwa ajili ya kuchimba kokoto na pia tunajenga kiwanda kwa ajili ya kutengeneza zege na tuko mbioni kuwa na kiwanda cha mabati na tutaanza kwa kazi za ndani za shirika," alisema Mkurugenzi wa Ujenzi wa NHC, Mhandisi Hekamen Mlekio.

Kwa upande wake Ofisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji wa Shelter Afrique, Andrew Chimphondah, alishukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ushirikiano inaounyesha kwa taasisi hiyo ikiwamo kutoa michango yake na kueleza kuwa, uamuzi wa kukutana na nchi wanachama kama Tanzania ina jitihada za kutekeleza azimio la Younde.



Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, mkoani Tabora wakiimba wimbo wa Taifa kabla ya kikao cha baraza kuanza.
**PICHA: VICENT TIGANYA**

## SAGCOT na TADB kuongeza thamani ya mazao nchini

**Na Beatrice Moses**

KITUO cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB) wamekubaliana kuwa na ushirikiano katika kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi nchini.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa SAGCOT, Geoffrey Kirenga, aliwaeleza waandishi wa habari juu ya makubaliano hayo baada ya mkutano kati ya watendaji wa SAGCOT na TADB uliofanyika jijini Dar es Salaam. Ujumbe wa TADB uliongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Frank Nyabundege.

"Tunaamini kwenye mabadiliko ya uongozi huwa kuna nguvu mpya ya kiutendaji, hivyo tutashirikiana na TADB katika kufanya mageuzi katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi nchini," alisema Kirenga na kueleza kuwa ujumbe wao uliipata nafasi ya kumweleza Mkurugenzi wa TADB namna Sagcot inavyofanya kazi na kuwa kuna haja ya kutengeneza ubia ambao utasaidia kukuza na kuendelea kilimo nchini kwa kuhakikisha mahitaji ya mkulima yanafikiwa ili kukifanya kilimo kuwa endelevu.

"Jukumu letu kubwa ni kuhakikisha wawekezaji katika sekta ya kilimo wanatambuliwa na wanatoa mchango kwenye mahitaji ya wakulima wadogo nchini. Tunaamini kwa kushirikiana na TADB tutaongeza ufanisi katika eneo hili," alisema Kirenga.

Nyabundege aliishukuru SAGCOT kwa mapokezi mazuri, na kwamba mwongozo waliopata kutoka SAGCOT utaiwezesha benki yao kuendeleza kwa urahisi na haraka juhudi za kuwasaidia wakulima na kukifanya kilimo kuwa cha kibiashara nchini.

"Ushirikiano kati yetu na SAGCOT utatuwezesha kuwafikia wakulima wengi zaidi katika maeneo tofauti nchini na kupelekea uzalishaji kuongeza," amesema Nyabundege.

# Serikali, Huawei kuendeleza wanawake sekta ya TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imeahidi kushirikiana na kuunga mkono jitihada za kampuni ya Mawasiliano ya Huawei katika kuweka mkazo zaidi na kuwaendeleza wanawake katika sekta ya TEHAMA ili kuongeza uwiano wa kijinsia kati ya wanawake na wanaume katika sekta hiyo.

Ahadi hiyo ya serikali ilitolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Zainabu Chaula, wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa mpango wa kuibua vipaji vya TEHAMA kwa vijana kupitia mafunzo vyuoni, ulioasisiwa na kampuni ya Huawei unaofahamika kama 'Seeds for the Future Program' iliyofanyika mwishoni mwa wiki jiji Dodoma.

Alisema serikali kwa kutambua umuhimu wa sekta ya TEHAMA, imejipanga kushirikiana na kampuni hiyo kuhakikisha inautumia vema mpango huo na mipango mingine kama hiyo kuzalisha vijana wenye weledi wa kutosha kuhusu masuala ya TEHAMA huku suala la usawa wa kijinsia pia likipewa kipaumbele.

"Tunaamini kupitia ushirikiano huu tunaoupata kutoka kwa wenzetu kampuni ya Huawei tutafanikiwa kukamilisha adhima hii. Pamoja na kuipongeza kampuni ya Huawei kwa kwa kutekeleza mpango huu kwa mwaka wa sita sasa naendelea kuwahakikishia ushirikiano mzuri zaidi kutoka serikalini ili kwa pamoja tufikie malengo," alisisitiza.

Aidha, Dk. Chaula alisema kuwa fursa nyingi zinapatikana kupitia TEHAMA na kati ya vijana 50 watakaopatiwa mafunzo hayo vijana 40 ni wasichana kitu ambacho kinatia moyo na kutoa hamasa kwa vijana hasa kutokana na ushuhuda wa moja ya wanufaika wa programu hiyo, Emilina Masanja kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe aliyasema hayo kupitia TEHAMA amekuza biashara yake kwa kuongeza wigo wa wateja ambao wengine wapo nje ya nchi.

Katika hatua nyingine, Dk. Chaula alitoa wito kwa vijana nchini kutumia vema maendeleo ya TEHAMA kwa kubuni fursa mbalimbali zinazoweza kutokana na sekta hiyo kwa maendeleo yao binafsi na maslahi mapana ya nchi ikiwamo mafunzo na fursa za ajira badala kutumia ukuaji wa sekta hiyo kufanya vitendo vilivyo kinyume cha maadili ya jamii na taifa kwa ujumla ikiwamo utapeli na makosa mengine kupitia mtandao.

Kwa upande wa Naibu Mkurugenzi Mkuu wa HUAWEI Tanzania, Tom Tao, alisema kuwa mafunzo hayo yameanza kutolewa mwaka 2016 kwa kuchagua wanafunzi 10 wa TEHAMA wanaofanya vizuri kutoka katika taasisi za elimu ya juu kwa kuwapatia mafunzo ya teknolojia za kisasa katika TEHAMA nchini China na pia kujifunza utamaduni wao.

Aliongeza kuwa kutokana na changamoto za UVIKO-19, kuanzia mwaka jana mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa kwa njia ya mtandao na idadi ya wanafunzi hao kuongezeka kutoka 10 hadi kufikia wanafunzi 50 ambapo mpaka sasa jumla ya wanafunzi 150 wamenufaika na programu hiyo.

# Mpango mabadiliko kidigitali sasa kuiletea fursa Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

MPANGO utakaoleta zana za kidijitali na vyanzo vya mafunzo ya kilimo kwa wakulima wadogo na biashara ndogo zinazojihusisha na kilimo barani Afrika umezinduliwa.

Mpango huo umeanzishwa kwa ushirikiano baina ya Mpango wa Microsoft 4Afrika na International Finance Corporation (IFC) unaolenga kupiga jeki mabadiliko ya kidijitali katika sekta ya kilimo-biashara barani Afrika, kuboresha mnyororo wa usambazaji na kukuza uzalishaji na pato la wakulima.

Kwa kuanzia, mfumo utakaotumia simu za mkononi utaanza kutumiwa na wakulima nchini Tanzania, Kenya, Nigeria, Cote d'Ivoire, na Uganda. Mpango huo umelenga kuwafikia na kusaidia wakulima 50,000 na vyama vya ushirika si chini ya 50. Mpango unakuja kutokana na ukweli kuwa teknolojia ya kidijitali uboresha uendeshaji wa mifumo ya minyororo ya uzambazaji katika mfumo wa chakula kupitia ufanisi mkubwa wa kilimo, uboreshwaji wa ufanyaji biashara, upatikanaji, huifadhi wa chakula na upatikanaji wa fedha.

Hata hivyo, matumizi ya zana hizi za kidijitali katika sekta ya kilimo barani Afrika bado ni madogo, kutokana na miundombinu, uwezo, uelewa, na mausala ya udhibiti. Kilimo kinachangia kiasi cha asilimia 25 ya pato la Afrika na uchangia asimilia 70 ya ajira zote.

"Sasa zaidi ya hapo awali, tunahitaji kuwa makini zaidi kwenye jinsi gani taasisi za kiteknolojia za kilimo zinafanya mabadiliko kidijitali, wanakutana na changamoto gani katika kupata teknolojia mpya, na changamoto za kila siku wanazoweza kuzipata katika eneo la maendeleo ya ujuzi wa kidijitali. Mkakati wa Microsoft 4Afrika ni kuwekeza katika teknolojia ya kilimo ili kufungua uwezo mahiri wa Afrika, kuleta ubunifu katika teknolojia ya kilimo, kuwekeza katika kilimo kitokanacho na takwimu ambacho kinaweza kuza mavuno, uzalishaji shambani na kukuza faida – vyote vikienda pamoja na kulisha taifa," alisema Kendi Nderitu, Meneja Mkazi wa Microsoft Kenya.

Ushirikiano huo unaongezea nguvu mifumo ya kipekee ya kidijitali ya Microsoft 4Afrika na Mradi wa Uongozi wa Kilimobiashara wa IFC ili kusaidia wakulima wadogo, vyama vyao, na "wauzaji wa mwisho" kupata taarifa na zana za kidijitali katika kukiongezea nguvu kilimo, kujenga taaluma ya biashara na kuboresha akiba ya chakula na upatikanaji wake katika mnyororo wote wa usambazaji.

Samuel Dzotefe, kaimu Mkurugenzi wa Viwanda wa Ukanda wa Mashariki ya Kati na Afrika uzalishaji, Kilimo-biashara na huduma, alisema:

"Teknolojia za kidijitali zina uwezo wa kukibadirisha kilimo kidogo barani Afrika. Kwa kuzifanya zana za kidijitali kupatikana kwa wakulima, vyama vya ushirika na wauzaji wa mwisho, Microsoft na IFC kwa pamoja zitasaidia sekta ya kilimo cha biashara kutumia fursa hii iliyoletwa na uchumi wa kidijitali."

Kiasi cha watu milioni 155 walipatwa na uhaba wa chakula kwa mwaka 2020 katika nchi 55, ongezeko la karibia watu milioni 20 kutoka mwaka 2019, kwa mujibu wa Ripoti ya Mwaka 2021 ya Janga la Chakula Duniani. Katika nchi 10 zenye idadi kubwa zaidi ya watu zinazokumbana na uhaba wa chakula, sita zilikuwa ni za Afrika.

Teknolojia ya kidijitali ni moja ya njia za kukuza uzalishaji wa kilimo na ufanisi. Ushirikiano huu utajumuisha mfumo wa kuchati wa simu wa Microsoft KuzaBot, ambao utaongeza kasi na kurahisisha utoaji wa taarifa muhimu kwa wakulima juu ya ufanyaji wa kilimo bora na biashara.

Mradi wa Uongozi wa Kilimobiashara wa IFC, ambao utakuwapo kwenye mfumo wa Microsoft wa mafunzo ya jamii, utasaidia wafanyabiashara wadogo, wakusanya mazao, na vyama vya wakulima kuboresha taaluma zao, uzalishaji, na uwezo wa ukopeshwaji. Kwa kipindi cha muda mrefu, ushirikiano unalenga kukuza zaidi uelewa wa sababu zinazopelekea utwaaji na utumiaji wa tatuzi za kidijitali miongoni mwa wakulima wadogo, vyama vya ushirika vya wakulima, na wadau wengine husika katika mnyororo wa usambazaji wa kilimo.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Zainab Chaula, akifungua mafunzo ya siku nane kwa wanafunzi 50 wa taasisi za elimu ya juu wanataaluma wa TEHAMA yanayotolewa na Kampuni ya Huawel Tanzania kupitia program yao ya Seeds for the Future jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafurahia DC kutatua kero uporaji ardhi

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

WAKAZI wa Kijiji cha Mwanadiratu wilayani Mkuranga, mkoani Pwani, wamepongeza juhudi zilizofanywa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Khadija Ally kwa kuwatatulia kero ya kuporwa ardhi na mwekezaji wa kigeni.

Pia wakazi hao wamedai kuvunjiwa nyumba zao na mwekezaji huyo.

Walisema hayo wakati wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti.

Sau Mdoe, mkazi wa kijiji hicho, alipongeza ziara iliyofanywa na Mkuu wa Wilaya hiyo kwa kufika kijiji hapo na kusikiliza kero za wananchi.

"Kwanza tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kututeulia mkuu wa wilaya, amekuja kijijini na kutusikiliza kero yetu ambayo imedumu zaidi ya miaka mitano bila kupatiwa majibu," alisema.

Alisema kuja kwake kumewapa matumaini na wana imani hata maeneo yao waliyoporwa na mwekezaji watarudishiwa.

Mkuu wa wilaya ambaye aliongozana na Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Mwantumu Mgonja na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo, alifanya mahojiano na pande zote mbili na kutilia shaka umiliki wa mwekezaji huyo.

Aliagiza serikali ya kijiji impelekee ofisini kwake hati za mauziano ya ardhi ikiwamo na kibali cha chuo uwekezaji nchini na mwekezaji anatakiwa awe nacho.

Pia, aliwataka wananchi waliobomolewa vibanda vyao bila makubaliano wamrushie nakala za matukio hayo katika simu yake ili afuatilie kwa kina na vyombo vyake vya uamuzi kabla hajafanya uamuzi wa kurejesha ardhi hiyo mikononi mwa wananchi.

# Wakulima waomba bima ya mazao

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAKULIMA wa tumbaku na pamba wilayani Kahama, mkoani Shinyanga wameziomba taasisi za fedha kuwapatia mikopo kwa ajili ya bima za mazao ili kufidiwa inapotokea hasara katika kilimo.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Emmanuel Charahani, aliyabainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kusaini mkataba wa utoaji wa bima ya afya kwa wakulima wa vyama vya ushirika kati Benki ya NBC, KACU na NHIF, kwa ajili ya wakulima wa mazao ya tumbaku na pamba.

Alisema msimu huu unaishia mwaka 2020/2021, tumbaku nyingi iliharibikia shambani kutokana na uwapo wa mvua iliyoambatana na upepo mkali na kusababisha wakulima kupata hasara ya Dola za Marekani 200,000 sawa na zaidi ya Sh. milioni 500.

Pia alisema vyama vya msingi vimeshindwa kulipa madeni waliyokopa katika taasisi za kifedha kwa ajili ya maandalizi ya kilimo baada ya kupata hasara iliyotokana na kunyesha mvua za masika.

Charahani alisema msimu huo walitarajia kununua kilo milioni tisa, lakini walinunua kilo milioni saba na kuziomba taasisi za fedha kwa kushirikiana na NHIF kuangalia uwezekano wa wakulima kuwa na bima za mazao kwa kuwa wana uwezo wa kuchangia gharama za bima hizo kupitia taasisi zao.

Mkuu wa kitengo cha wateja wadogo wa benki ya NBC, Raymond Urassa, alisema wataendelea kutoa mikopo ya bima ya afya kwa wakulima wa mazao ya tumbaku na pamba kwa wale waliojiunga na vyama vya msingi lengo likiwa kutatua shida za gharama za matibabu.

Alisema licha ya kutoa mikopo ya bima ya afya wapo tayari kuwakopesha wakulima wa zao la pamba na tumbaku bima ya mazao ambayo itawasaidia kuondokana na hasara wanayopata wakati wa kilimo na baada ya mavuno.

Mkurugenzi wa huduma kwa wanachama wa NHIF, Christopher Mapunda, alisema wamefanya maboresho kwenye vituo vya afya na maduka ya dawa.

# HakiElimu yapiga jeki watoto wa kike

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

TAASISI ya Hakielimu imetoa msaada wa vyerehani vya kushonea taulo za kike (SODO) kwa wanafunzi wa kike wanaosoma shule za msingi na sekondari wilayani Masasi ili kusoma kwa utulivu.

Msaada huo ulitolewa wilayani Masasi kupitia mradi wake wa JRTI, ambao unalenga kuwajali watoto hasa wa kike waliopo mashuleni na nje ya shule, huku ikieleza kwamba lengo la kutoa vyerehani hivyo ni kuhakikisha watoto wa kike waliopo shuleni wanasoma bila ya kukatisha masomo darasani au kuingia katika utoro kwa sababu ya kuwa katika siku zao.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, mratibu wa HakiElimu wilayani Masasi, Blandina Nakajumo, alisema utakuwa mkombozi wa wanafunzi wa kike wa shule za msingi na sekondari.

Nakajumo alisema upatikanaji wa vyerehani hivyo vitawawezesha watoto wa kike kukaa darasani na kusoma kwa utulivu.

NIPASHE JUMATATU SEPTEMBA 6, 2021
Nipashe
Spotika




USAJILI 10 BORA WA MAJIRA YA JOTO 2021 UK. 12




# NYOTA WATANO PSG WAKUMSAIDIA MESSI

**PARIS, Ufaransa**

KATIKA usajili wa kushangaza wa majira haya ya joto, PSG ilimpata gwiji wa Barcelona, Lionel Messi, kwa uhamisho wa bure baada ya 'Blaugrana' hao kushindwa kumwongezea mkataba.

Miamba hao wa Ligue 1 sasa wana kikosi chenye nyota wenye ubora karibu kila eneo la uwanja, haswa mbele, ambapo Messi anapangwa kuungana na Neymar na Kylian Mbappe.

Raia huyo wa Argentina bila shaka ndiye mchezaji bora aliyepamba mchezo huo, anatarajiwa sana kupiga hatua na kuifanya PSG kuwa timu bora nchini Ufaransa na Ulaya.

Lakini hii ni mara ya kwanza kwa Messi kutua katika klabu nyingine zaidi ya Barcelona, na amewasili PSG bila mazoezi yoyote ya kabla ya msimu. Hiyo ni kwa sababu mchezaji huyo alikuwa likizo baada ya Argentina kubeba Kombe la Copa America 2021.

Halafu aliwasili Barcelona akitarajia kuongezewa mkataba wake kabla ya msimu mpya, kitu ambacho hakikutokea.

Messi, kwa sifa yake, atakuwa na wachezaji wenzake kadhaa wa PSG ambao wanaweza kuchukua shinikizo kutoka kwake katika mazingira yake mapya. Kwenye makala haya tunaangalia wachezaji watano ambao wanaweza kumsaidia Messi kukaa PSG, twende sasa...

**#5. Gianluigi Donnarumma**

Gianluigi Donnarumma ni mmoja wa makipa wachanga kwenye mchezo huo kwa sasa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, alicheza vizuri sana kwenye michuano ya Euro 2020 wakati Italia ikibeba ubingwa huo.

Kabla ya ushujaa wake kwenye Euro, Donnarumma alicheza msimu wake wa sita kwa AC Milan na akiiwezesha kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka kumi.

Donnarumma sasa anaonekana kuwa na jukumu la kuchukua mikoba ya golikipa mkongwe, Keylor Navas, na anaweza kupiga hatua katika mazingira yake mapya, ambayo yataondoa shinikizo kwa Messi na wageni wengine mashuhuri wa msimu wa huu wa majira ya joto klabuni hapo.

**#4. Marquinhos**

Marquinhos, anayechukuliwa kama mmoja wa walinzi bora wa kati katika mchezo huo, amekuwa PSG kwa karibu miaka kumi. Ingawa PSG wana orodha ya nyota, haswa mbele, kampeni hii, ulinzi wao una sura mpya. Hapa ndipo uwapo wa Marquinhos unapofaa.

Ndio kwanza ana umri wa miaka 27, alitinga fainali ya Copa America 2021 akiwa kiongozi wa Brazil na anaweza kufunga, na hilo litapunguza shinikizo kwa wachezaji wapya wa PSG kama Messi na Sergio Ramos.

**#3. Marco Verratti**

Marco Verratti, ambaye alikuwa sehemu ya kampeni ya ushindi ya Euro 2020 na kikosi cha Italia, amekuwa PSG kwa karibu miaka kumi.

Anachukuliwa kama mmoja wa viungo bora zaidi kwenye mchezo huo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, anatarajia kuendelea na kiwango chake bora msimu huu wa 2021-22 pale PSG.

Amecheza karibu mechi 350 kwenye mashindano yote hapo PSG, akifunga mara tisa tu, lakini akitoa pasi za mabao 58. Akiwa mshindi mara saba wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, atakuwa msaada mkubwa kwa wachezaji wageni hasa Messi msimu huu.

**#2. Kylian Mbappe**

Ni nani bora zaidi kuweza kuondoa shinikizo la Messi pale PSG kuliko mtu yeyote kama Kylian Mbappe, anayechukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi vijana kwa sasa.

Nyota huyo wa Ufaransa alikuwa na wakati mbaya kwenye michuano ya Euro 2020, baada ya kukosa penalti na kuwafanya Ufaransa kutolewa kwenye raundi ya 16 bora na Uswisi. Lakini Mbappe alikuwa na kampeni nzuri ya msimu wa 2020-21.

Alifunga mabao 42 katika mashindano yote wakati wababe hao wa Ligue 1 waliposhindwa kubeba ubingwa wa ligi na waliondolewa kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Manchester City.

Ana umri wa miaka 22, mshindi wa Kombe la Dunia mwaka 2018, ametoa mchango wa mabao 200 (mabao 133, asisti 63) katika michezo 174 tu ya PSG.

Licha ya uvumi juu ya kutaka kuondoka, Mbappe yuko tayari kukaa klabuni hapo na kuanzisha ushirikiano wa kuvutia kati yake na Neymar na Messi msimu huu.

**#1. Neymar**

Neymar aliripotiwa kuwa na jukumu muhimu katika kumleta Messi PSG. Kwa hiyo raia huyo wa Brazil anakaribia kuanza msimu wake wa tano na wababe hao wa Ligue 1, na anatarajiwa kuchukua jukumu muhimu katika kumfanya rafiki yake mzuri ajisikie yuko nyumbani katika mazingira yake mapya.


Mapema huko Barcelona, Neymar alianza ushirikiano mkubwa na Luis Suarez na Messi pale mbele, akishinda mataji mawili ya Ligi Kuu ya Hispania.

Ingawa Suarez hayupo PSG, Messi na Neymar, pamoja na Mbappe, wanatarajiwa kufunga mabao mengi na kuwasaidia miamba hiyo ya Ligue 1 mwishowe kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Neymar anaweza kuwa msaada mkubwa zaidi kwa Messi kufanya mabadiliko katika kikosi hicho.

## ISIKUPITE

KIPA wa Manchester United, David De Gea, ndiye golikipa aliyemaliza mechi nyingi (124) bila kuruhusu 'clean sheets' kwa muongo uliopita, akifuatiwa na Hugo Lloris (Tottenham - 108), Joe Hart (Manchester City-West Ham-Burnley - 98), Petr Cech (Chelsea na Arsenal - 95) na watano akiwa ni Ederson (Manchester City - 75).



## Extra Time

# USAJILI 10 BORA WA MAJIRA YA JOTO 2021



Cristiano Ronaldo

**LONDON, England**

DIRISHA la uhamisho wa wachezaji kipindi cha majira ya joto kwa mwaka 2021, lilikuwa moja ya madirisha makubwa katika miaka ya hivi karibuni.

Pamoja na matatizo ya kifedha yaliyotokana na janga la ugonjwa wa COVID-19, klabu nyingi hazikusita kujitokeza ili kufikia malengo yao. Kwa kweli, kama mwaka 2020, mikataba ya mkopo iliendelea kuwa njia inayopendelewa ya biashara kwa klabu nyingi.

Wachezaji wachache wa hali ya juu walichagua njia hii kuhamia kwenye malisho mapya ya msimu huu wa joto. Wengi wao walifanya hivyo kutafuta changamoto tofauti au baada ya kuwa ziada ya mahitaji katika klabu zao za awali.

Makala haya yanaangalia usajili 10 bora kwenye dirisha la uhamisho lililomalizika hivi karibuni, shuka nayo sasa...

#10. Antoine Greizmann (Barcelona kwenda Atletico Madrid)

Baada ya kuwa na misimu miwili mibaya kule Barcelona, Antoine Griezmann amerudi kwenye uwanja wake wa zamani pale Atletico Madrid.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2018, aliwasili na shangwe nyingi kule Camp Nou katika msimu wa joto wa mwaka 2019. Lakini Mfaransa huyo alikuwa na kampeni ya kwanza ya kusikitisha katika uwanja wake mpya, akifunga mara 15 tu na kutoa asisti nne katika michezo 50 kwenye mashindano yote.

Griezmann alionekana kuimarika baada ya kuwasili kwa kocha, Ronald Koeman msimu uliopita, akifunga mabao 20 na asisti 13. Pamoja na kuondoka kwa gwiji wa klabu hiyo, Lionel Messi msimu huu wa joto, Mfaransa huyo alitarajiwa kuongoza safu ya ushambuliaji ya Barcelona. Lakini baada ya kuwasili kwa nyota mpya, Memphis Depay kulimfanya Griezmann kutokuwa kwenye mahitaji zaidi.

Alizomewa hata na mashabiki wa Barcelona katika mchezo ambao ulionekana kuwa wa mwisho kwake katika klabu hiyo. Griezmann, ambaye amekuwa akihusishwa na kuondoka majira yote ya joto, alijiunga na Atletico kwa mkopo siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ambaye ameifungia Atletico mabao 133 katika michezo 257, ataungana na mchezaji mwenzake wa zamani wa Barcelona, Luis Suarez.

**#9. Eduardo Camavinga (Rennes kwenda Real Madrid)**

Anatajwa kama mmoja wa viungo bora wakabaji kwa sasa, Eduardo Camavinga amehama kutoka Rennes kwenda LaLiga katika Klabu ya Real Madrid.

Camavinga alianza kucheza mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, akiwa na umri wa miaka 16 tu msimu wa 2018-19. Aliwasili Real Madrid huku akiwa pia anawaniwa na Manchester United, Liverpool, Arsenal na PSG.

Camavinga anatajwa kama anakwenda kuchukua nafasi ya Luka Modric ambaye kwa sasa umri unamtupa mkono.

**#8. Jack Grealish (Aston Villa kwenda Manchester City)**

Baada ya kutamba sana kule Aston Villa, ilionekana ni suala la muda tu kabla ya Jack Grealish kuhamia klabu kubwa.

Hiyo ilifanyika msimu huu wa majira ya joto wakati mabingwa wa Ligi Kuu England, Manchester City walipolipa kiasi cha pauni milioni 100 kuinasa saini ya kiungo huyo. Katika mchakato huo, Grealish alikuwa mchezaji ghali zaidi katika mpira wa miguu kwenye historia ya soka la Uingereza.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, ametoa mchango wa mabao 32 (akifunga 14, asisti 18) katika kipindi cha misimu miwili iliyopita ya Ligi Kuu England. Kiungo huyo mkabaji hodari pia alionyesha kiwango cha kuvutia kwenye michuano ya Euro 2020 ambako hakupata nafasi nyingi za kucheza.

**#7. Romelu Lukaku (Inter Milan kwenda Chelsea)**

Romelu Lukaku ni mmoja wa washambuliaji bora kwenye mchezo huo kwa sasa. Mbelgiji huyo amerejea Chelsea baada ya misimu miwili ya kuvutia kule Serie A akiwa na Inter Milan.

Lukaku alitoa mchango wa mabao 80 (mabao 64, asisti 16) akiwa na Nerazzurri hao. Lakini kwa sababu ya shida zao za kifedha, Inter ililazimika kumuuza nyota huyo kwa thamani ya euro milioni 115 msimu huu wa majira ya joto.

Lukaku, ambaye alifurahia kampeni nzuri kwenye michuano ya Euro 2020, kwa mara ya mwisho aliichezea Chelsea mwaka 2013, na sasa anatarajiwa kuwa mchezaji muhimu katika harakati za 'Blues' kuwania taji la Ligi Kuu msimu huu.

**#6. Raphael Varane (Real Madrid kwenda Manchester United)**

Raphael Varane, mmoja wa walinzi bora kabisa kwa sasa, alimaliza ushirika wake wa miaka kumi akiwa na Real Madrid msimu huu wa majira ya joto kwa kuhamia Manchester United.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2018 aliwasili Old Trafford akiwa ameshinda mataji matatu ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kule Madrid.

Akijulikana kwa nguvu, kasi na umahiri wa kucheza mpira, Varane anaonekana kama mchezaji bora kumsaidia nahodha Harry Maguire pale Man United.

Varane ameanza maisha mazuri kwenye Ligi Kuu England wakati timu yake iliposhinda bao 1-0 dhidi ya Wolves.

#5. Jadon Sancho (Borussia Dortmund kwenda Manchester United)

Jadon Sancho ni mmoja wa mawinga wachanga wanaofurahisha zaidi kwenye mchezo huo kwa sasa.

Baada ya kutengeneza jina lake kama mchezaji wa kiwango cha dunia wakati wa msimu wake uliofanikiwa sana kule Borussia Dortmund, Sancho alinyakuliwa na Manchester United. Klabu ya Old Trafford ilitoa karibu milioni 100 kwa mchezaji huyo ili ampate baada ya harakati za mwaka mzima.

Sancho, ambaye alitoa michango ya mabao 114 kule Dortmund, ameanza maisha ya kawaida pale Old Trafford. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, alianza kuichezea United mwishoni mwa wiki iliyopita, lakini bado hajafunga bao au kutoa asisiti yoyote katika michezo mitatu.

**#4. Achraf Hakimi (Inter Milan kwenda PSG)**

Achraf Hakimi ni mmoja wa mabeki wa pembeni wafungaji wazuri kwenye mchezo huo. Mara ya kwanza raia huyo wa Morocco alitengeneza jina lake kule Borussia Dortmund wakati akicheza kwa mkopo kutoka Real Madrid.

Hakimi alifurahia msimu mzuri kwenye Ligi Kuu Italia ambako alifunga mabao saba na kutoa asisti kumi akiwa na Inter Milan. Sasa amewasili kwa uhamisho wa Euro milioni 60 kutoka kwa mabingwa hao wa Serie A kwenda PSG.

**#3. Gianluigi Donnarumma (AC Milan kwenda PSG)**

Mmoja wa magolikipa wanaofurahisha zaidi kwenye mchezo huo kwa sasa, Gianluigi Donnarumma amewasili PSG kwa uhamisho wa bure msimu huu wa majira ya joto. Amepigiwa upatu kufuata nyayo za kipa mwenzake mashuhuri, Gianluigi Buffon.

Baada ya msimu wa sita na AC Milan, Donnarumma alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu katika kampeni ya ushindi ya Euro 2020 akiwa na kikosi cha timu ya Taifa ya Italia. Aliokoa penalti dhidi ya Hispania kwenye nusu fainali na England kwenye fainali.

Bado hajacheza mechi yake ya kwanza pale PSG baada ya kujiunga na klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto. Lakini haitachukua muda mrefu kabla ya Donnarumma kuchukua wadhifa kutoka kwa mkongwe Keylor Navas.

**#2. Cristiano Ronaldo (Juventus kwenda Manchester United)**

Cristiano Ronaldo amerudi Manchester United baada ya miaka tisa ya utukufu kule Real Madrid na misimu mitatu pale Juventus.

Alikuwa akitarajiwa sana kuondoka pale 'Bianconeri' msimu huu wa majira ya joto, Ronaldo alipigiwa upatu kutua Manchester City. Lakini katika hali ya kushangaza, klabu yake ya zamani ya Man United iliingilia kati kwenye kinyang'anyiro hicho na kumnyakua mchezaji huyo.

Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, ni mshindi mara tano wa Ballon d'Or na Ligi ya Mabingwa, anatarajiwa kuwaongoza 'Mashetani Wekundu' hao katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu.

Alikuwa pia na kampeni nzuri kwenye michuano ya Euro 2020, akifunga mabao matano.

**#1. Lionel Messi (Barcelona kwenda PSG)**

Katika usajili mkubwa ambao hakutarajiwa msimu huu wa majira ya joto ni hadithi ya Barcelona na Lionel Messi, ambaye amehamia PSG kwa uhamisho wa bure.

Baada ya kampeni ya ushindi wa Kombe la Copa America 2021, Messi alitarajiwa sana kusaini nyongeza ya mkataba na 'Blaugrana' hao. Lakini hiyo haikutokea, kwani Barcelona ilishindwa kutokana na sheria za kifedha za LaLiga licha ya Messi kukubali kukatwa asilimia 50 ya mshahara wake.


Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or - ambaye alitoa mchango wa mabao 1100 kule Barcelona, alianza kuichezea PSG kwa mara ya kwanza wikendi iliyopita.

## Nukuu


"Kumsajili [Cristiano] Ronaldo ni vizuri kwa mashabiki. Mfalme amerudi, lakini inanikatisha tamaa. Unauza jezi na Ronaldo. Unashinda ligi na Kane [Harry]. Nilisema kupitia Sky siku moja kwamba Ronaldo ni nusu ya mchezaji ambaye alikuwa awali. Mashabiki wa United hawapendi hilo. Lakini huo ni ukweli tu. Hataweza tena kuwapita wachezaji watatu kupiga kona ya juu. Kwa fedha walizotumia kwa Jadon Sancho na Ronaldo, hakika unajaribu kumpata Kane," **nyota wa zamani wa Arsenal, Paul Merson**



"Katika kazi yangu, nilikuwa nikikosa barafu ya keki: Kucheza na Leo [Messi] kwenye klabu. Nilikuwa na nafasi kadhaa za kwenda Barca. Inanifurahisha kuwa naye kila siku na kuona anachofanya na si tu tunapokuwa naye timu ya Taifa ya Argentina," **Angel Di Maria akizungumzia Messi kutua PSG**



"Nilikuwa sina uhakika kama nitapata tena jezi namba saba, hivyo napenda kutoa shukrani kwa Edi (Cavani) kwa uamuzi wake wa kukubali kuiachia," **mshambuliaji mpya wa Manchester United, Cristiano Ronaldo**



# VITA VYA MAKOCHA 10 WA KIGENI LIGI KUU 2021/22

**Na Adam Fungamwango**

RATIBA ya Ligi Kuu inatarajiwa kutoka wiki Ijayo kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo. Na baada ya hapo kila timu itajua itaanza na nani. Hakika itakuwa ni vita ya timu 16 kuwania ubingwa wa Tanzania Bara msimu wa 2021/ 22.

Inatarajiwa kuwa Ligi Kuu ya aina yake kutokana na udhamini mkubwa, ikiwamo kupungua kwa idadi ya timu. Msimu uliopita zilikuwa timu 18, lakini msimu ujao zitakuwa 16. Tumeona klabu zikijizatiti kusajili wachezaji bora. Hata hivyo, kusajili wachezaji bora ni jambo moja na kutengeneza timu ni jambo lingine.

Kazi hiyo ni ya benchi la ufundi, hivi sasa makocha wako kwenye pilikapilika ya kuvisuka vikosi vyao kwa ajili ya msimu mpya wa mashindano. Makocha ndiyo mhimili wa timu nadiyo wanaotengeneza mifumo mbalimbali na kuvifanya vikosi vyao kuwa imara. Hawa ni makocha watakaoonyeshana kazi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu 2021/22...



Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, akiwa mazoezini na kikosi chake.

**#1. Didier Gomes - Simba (Mfaransa)**

Ni kocha wa mabingwa wa nchi. Raia huyo wa Ufaransa ameipa Simba ubingwa msimu huu, ingawa hakuanza nayo. Aliichukua timu hiyo kutoka kwa kocha Mbelgiji Sven Vandenbroeck. Hakubadili gea, aliendelea nayo na moto ule ule, na si kwenye Ligi Kuu tu, hata Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa sasa ameanza nayo timu tangu mwanzo, amesajili mwenyewe, hata hivyo pamoja na kupoteza wachezaji Luis Miquissone na Clatous chama, bado anatarajia kuleta upinzani mkali kwa timu zingine.

**#2. Nasreddine Nabi - Yanga (Mtunisia)**

Aliianza kuifundisha Yanga, baada ya kutimuliwa kwa kocha raia wa Burundi, Cedrick Kaze. Kocha huyo raia wa Tunisia, kwa muda mfupi alioingia msimu uliopita, aliifanya Yanga kushinda mechi nyingi mfululizo.

Tatizo lilikuwa ilishatoka sare nyingi, hivyo kushindwa kabisa kuikuta Simba kileleni. Msimu huu amehusika kwenye usajili, anaiandaa timu tangu mwanzo mwenyewe akitarajia kwenda kuipa Simba wakati mgumu kutetea taji lake.

**#3. George Lwandamina - Azam (Mzambia)**

Angalau sasa Azam FC imetulia baada ya ujio wa kocha huyu wa zamani wa Yanga. Baada ya kuvurunda kwenye mechi kadhaa za msimu uliopita, viongozi wa Azam walimleta kocha huyo ambaye alianza kusajili wachezaji anaowahitaji kipindi cha dirisha dogo. Timu ikakaa vizuri.

Sasa amesajili na anaitengeneza timu yake kwa ajili ya msimu ujao. Ni moja kati ya timu inayotarajiwa kuleta upinzani na hata kutwaa ubingwa msimu ujao.

**#4. Patrick Okumu - Biashara United (Mkenya)**

Okumu ni mmoja wa makocha waliojipatia sifa kwa muda mfupi tu baada ya kujiunga na Biashara United. Alichukuliwa baada ya kocha Francis Baraza kwenda Kagera Sugar.

Alishikilia uzi ule ule wa Mkenya mwenzake, na kuipeleka Biashara United kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika. Msimu huu anatakiwa kuthibitisha kuwa hakutembelea nyota ya mwenzake.

**#5. Melis Melo - Coastal Union (Marekani)**

Coastal Union wamemchukua kocha kutoka Marekani, ambaye amezifundisha timu kadhaa nchini Kenya. Melis Melo, ndiye kocha mkuu wa sasa wa timu hiyo akishika nafasi ya Juma Mgunda, ambaye amekuwa Mkurugenzi wa Ufundi. Wengi wanataka kuona kocha huyo mpya nini atakifanya kwenye timu hiyo.

**#6. Etienne Ndayiragije - Geita Gold (Burundi)**

Huyu ni kocha mzoefu na maarufu nchini, aliwahi kuwa kocha wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars. Alizifundisha pia timu za Mbao na KMC. Itakumbukwa aliwahi kuifanya Mbao FC kutoka kuwa timu ndogo na kuwa tishio.

Sasa ataiongoza Geita Gold iliyopanda daraja msimu huu. Ila anatakiwa kukumbuka kuwa rekodi inaonyesha kuwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kila msimu. Timu moja iliyopanda daraja ni lazima ishuke.

**#7. Francis Baraza - Kagera Sugar (Mkenya)**

Mkenya huyu aliifanya Biashara United kuwa moja ya timu tishio tangu ipande Ligi Kuu. Aliondoka kwenye timu hiyo na kwenda Kagera Sugar kwa ajili ya kazi moja tu. Kuinusuru isishuke daraja. Na kweli alifanikiwa. Kwa sasa anaiandaa kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu. Anatarajia kuleta ushindani mkubwa kwa klabu zingine.

#8. Mathias Lule - Mbeya City (Mganda)

Kocha huyu Mganda msimu uliopita aliinusuru Mbeya City kushuka daraja. Ndiyo maana hadi leo yupo kwenye klabu hiyo. Anatarajia kuiongoza tena timu hiyo kwa ajili ya msimu ujao. Ni kocha mwenye mbinu na mwenye uwezo wa kusoma mfumo wa timu pinzania, akaufanyia kazi.


**#9. Haruna Hererimana - Mbeya Kwanza (Mrundi)**

Ni kocha raia wa Burundi, lakini si mgeni sana kwenye soka la Tanzania. Aliwahi kuzifundisha timu za Lipuli na KMC. Amepewa mikoba ya kuifundisha Mbeya Kwanza ambayo itacheza kwa mara ya kwanza Ligi Kuu Tanzania Bara.

**#10. Thierry Hitimana - Mtibwa Sugar (Mnyarwanda)**

Aliwahi kuifundisha Biashara United, halafu akatimkia Namungo, akaenda Mtibwa Sugar, lakini hakukaa sana na sasa amerudishwa Mtibwa Sugar. Ni mmoja wa makocha wazoefu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo anategemewa kutoa upinzani mkubwa kwa makocha wenzake.

**JE, WAJUA?**




Ecuador ndiyo timu pekee ya taifa ambayo Lionel Messi ameifunga mabao mengi (6) zaidi akiichezea Argentina, lakini ni moja kati ya timu nne alizofanikiwa kufunga hat-trick dhidi yake. Timu zingine alizofunga mabao mengi akiwa na timu ya taifa ni Uruguay, Chile, Paraguay na Brazil, kila moja akiifunga mabao matano.



# Tamasha la Wabunge, NMB lamkuna Mpango

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Phillip Mpango, amesifu malengo chanya ya Tamasha la NMB na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kufichua kuwa yamewavutia Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, licha ya kutohudhuria kwao kutokana na sababu mbalimbali.

Tamasha hilo lililotambulika kama 'NMB Kivumbi na Jasho', lilifanyika mwishoni mwa wiki jijini Dodoma, likianza na matembezi ya hisani kuanzia viwanja vya Bunge hadi viunga vya Chinangali Park, ambako Dk. Mpango aliyekuwa mgeni rasmi, alipokea mchango wa NMB wa kuboresha elimu jijini Dodoma wenye thamani ya Sh. milioni 17 kutoka benki hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka.

Tamasha la Kivumbi na jasho, lilihudhuriwa na wabunge wote walioongozwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, mke wa Makamu wa Rais, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene na mawaziri mbalimbali.

Mchango huo uliotolewa na Benki ya NMB ni rimu za karatasi bunda 1,500 zenye thamani ya Sh. milioni 15 na taulo za kike zenye thamani ya Sh. milioni mbili maalumu kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la saba waliopo kwenye makambo wakijiandaa na mtihani wa darasa la saba.

Akizungumza kabla ya kumkabidhi mchango huo, Dk. Mpango, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alimweleza Makamu wa Rais kuwa Benki ya NMB imetumia tamasha la NMB na Wabunge, kuzindua mpango endelevu wa kuchangia maendeeleo ya Watanzania kwa kutazama mahitaji ya eneo husika ambapo michango hiyo itafanyika kila baada ya miezi mitatu.

Kwa Jiji la Dodoma, mpango huo umelenga kuchangia zaidi utatuzi wa changamoto za elimu, pamoja na 'Mpango Mkakati' wa kuligeuza jiji hilo kuwa la kijani kupitia upandaji miti na utunzaji mazingira.

"Leo kupitia tamasha hili, tunazindua programu hiyo endelevu, itakayokuwa inafuata kalenda ya vikao vya Bunge hapa Dodoma, ili kila litakapofanyika tamasha hilo, wabunge wote wawe sehemu ya washiriki. Kila tutapokutana hapa tutakuwa na kauli mbiu maalum inayolenga kusaidia jitihada za serikali katika kuboresha elimu," alisema Zaipuna.

"Kwa kuanzia, leo tunamkabidhi Mkuu wa Mkoa rimu za karatasi 1,500 na taulo za kike, kwa ajili ya wanafunzi wa mkoa wake wanaojiandaa na kambi za mitihani. Habari njema ni kuwa, tamasha hili limeanzia Dodoma, ila litasambaa kote nchini na tamasha lijalo hapa litakuwa majira ya mvua na tutalitumia kupanda miti kuibadili Dodoma kuwa ya kijani," alisisitiza Zaipuna.

Aidha, Zaipuna alimhakikishia Dk. Mpango kuwa NMB ni benki bora na imara, yenye mtaji mkubwa na weledi wa kutosha kuhakikisha wateja wao na Watanzania wanapata huduma rafiki, huku akiishukuru Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa jinsi inavyoshirikiana nao katika kuifanya kuwa benki ya kipekee nchini.

Naye Dk. alisema Rais Samia na Waziri Mkuu Majaliwa, pia wamevutiwa nayo na walitamani kuwa sehemu ya washiriki, lakini majukumu waliyonayo yamewakwamisha.

"Binafsi nalishukuru Bunge kwa kunialika kuja hapa, Rais Samia na Waziri Mkuu Majaliwa nao wamevutiwa na hiki na walitamani kuja, Ila wamebanwa, na wakaniagiza nifikishe kwenu NMB na wabunge salamu zao.



Katibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Wakili Dunford Mpelumbe (kushoto), akimpa maelezo Mkuu wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Watoa Huduma katika sekta ya mafuta na gesi Tanzania (ATOGS) , Sebastian Balthoromew, alipofika Bungeni kikazi mwisho wa wiki jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Agizo maabara bubu kufungwa

Na Augusta Njoji, DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imewaagiza waratibu wa huduma za maabara wa mikoa na halmashauri kuhakikisha wanazifungia maabara bubu zinazoendeshwa kinyume na utaratibu.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, anayeshugulikia Afya, Dk. Grace Magembe, alitoa agizo hilo jana alipokuwa akifunga kikao kazi cha waratibu wa huduma za maabara wa mikoa na halmashauri jijini hapa.

Alisema maabara bubu kwa sasa hazitakiwi kuwapo kwa kuwa kwa sasa serikali imejipanga kuhakikisha inatoa huduma bora za afya kwa jamii.

Naibu Katibu huyo alishangaa kuona kuna viongozi mbalimbali katika ngazi ya Kata, Halmashauri na Mkoa, lakini bado kunakuwa na maabara bubu.

"Nyie viongozi timizeni majukumu yenu kwa kuhakikisha maabara hizo zinafungiwa kwa kuwa zinachafua taaluma ya maabara nchini," alisema.

Aliwataka kuhakikisha maabara inayosajiliwa na kutambulika na serikali ifanye kazi ikiwa na wataalamu wenye ujuzi, weledi na kutoa vipimo ambavyo vinasaidia kuwapa matibabu wananchi.

"Zoezi hili la kuzikagua maabara bubu ziendane sambamba na maabara za watu binafsi, pamoja na maabara za Serikali, kwa kuwa maabara zote zinatakiwa kufanyakazi kwa kuzingatia vigezo na masharti ya kitaaluma," alisisitiza.

Kuhusu kero za wananchi, Dk. Maghembe aliwataka kuhakikisha wanashughulikia kero za wananchi kwa kuwasikiliza na kusimamia utoaji wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Pia aliwataka kuhakikisha wanasimamia utoaji wa huduma bora kwa wananchi kwa kuangalia umahiri wa watumishi wa maabara ili kujua taaluma na uwezo wao katika kutoa huduma hiyo kwa jamii, kwa kuwa serikali inahitaji kutoa huduma bora na kutoa vipimo sahihi.

# NEMC yapewa kongole usimamizi mzuri miradi

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, ameipongeza Mamlaka ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kwa usimamizi mzuri wa mazingira kwenye miradi iliyopo mkoani Dodoma.

Jafo alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki alipotembelea dampo la Chidaya, mabwawa ya maji taka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Hospitali ya Benjamin Mkapa ili kuangalia utekelezaji wa maelekezo aliyoyataoa miezi sita iliyopita.

Waziri alielezea kufurahishwa kwake na utekelezaji wa maagizo hayo kazi ambayo yamefanywa na NEMC kwa kushirikiana na wadau wengine wa mazingira kwa kuhakikisha masuala ya mazingira yanadhibitiwa ipasavyo.

Katika ziara hiyo, Waziri Jafo alibainisha kuwa maagizo hayo aliyoyatoa mwezi wa nne mwaka huu na kuipongeza NEMC Kanda ya Kati kwa usimamizi na ufuatiliaji mzuri ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa maagizo hayo.

"NEMC mmefanya vizuri sana kwenye kusimamia mazingira mkoani Dodoma nawapongeza sana na nawaomba mshikilie hapohapo hakikisheni kwenye masuala ya mazingira watu wanafuata sheria na miongozo iliyopo," alisema Waziri Jafo.

Waziri Jafo aliwataka wasimamizi wa mradi huo wa dampo kuhakikisha ukuta waliojenga unadumu kwa muda mrefu ili wananchi wa Dodoma waendelee kuwa salama bila kuathiriwa na majitaka ambayo yatatiririka wakati wa mvua.

Waziri Jafo aliwataka wasimamizi hao kulitumia vizuri dampo hilo na kuhakikisha taka zote zinazotupwa hapo zinashindiliwa vizuri ili zisisambae ovyo na kuleta uchafuzi wa mazingira.

Naye Meneja wa Kanda hiyo wa NEMC, Dk. Flanklin Rwezimula, ambaye aliambatana na waziri kwenye ziara hiyo, alisema mawasiliano ya mara kwa mara kati ya Baraza hilo na DUWASA yamefanikisha utekelezaji wa maelekezo hayo.

Akitoa taarifa kuhusu utekelezaji wa maelezo ya awali, Meneja wa Dampo la Chidaya, John Kiwanga, alisema mara baada ya kupokea maelekezo ya Waziri Jafo kupitia kwa Mkurugenzi wa Jiji waliyafanyia kazi mara moja na kujenga ukuta huo.

"Kama unavyoona mheshimiwa waziri hapa tumejenga ukuta huu kwa matofali ya kawaida tu na hatua hii itasaidia sana kuzuia majitaka kutoka katika dampo hili kutototoka nje na kuchafua vyanzo vya maji," alisema Kiwanga.





Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), akikagua mbegu za mazao mbalimbali zilizofanyiwa utafiti na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) kituo cha Uyole, jijini Mbeya, alipotembelea kituo hicho mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TARI kuvuna magunia 2,500 mbegu za ngano

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole jijini Mbeya, inatarajia kuvuna zaidi ya magunia 2,500 ya mbegu za ngano ambayo yatasambazwa kwa wakulima wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na baadhi ya mikoa ya Kanda ya Kati ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo nchini.

Mbegu hizo ni miongoni mwa mikakati ya serikali kuhakikisha nchi inajitosheleza kwa ngano na kupunguza kiwango cha uagizwaji kutoka nje ya nchi.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Dk. Tulole Bucheyeki, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa uvunaji wa ngano hizo uliofanywa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, kwenye mashamba ya taasisi hiyo.

Dk. Bucheyeki alisema kwa sasa asilimia 90 ya ngano zinazotumika nchini zinaagizwa kutoka nje ya nchi na uwezo wa Tanzania kuzalisha zao hilo ni asilimia 10 pekee jambo ambalo alisema sio sahihi kutokana na kuwa na ardhi inayoruhusu zao hilo kustawi.

Alisema wamefanya utafiti na kuzalisha mbegu za aina tatu ambazo zinafaa kulimwa nchini na mbegu hizo wamezizalishwa kwa wingi kwa ajili ya kuwasambazia wakulima.

Alizitaja aina hizo za mbegu kuwa ni Sifa yenye uwezo wa kuzaa magunia 40 mpaka 55 kwa hekta, Merina yenye uwezo wa kuzaa gunia 45 mpaka 45 kwa hekta na Ngoli ama Mwali yenye uwezo wa kuzaa magunia 34 mpaka 40 kwa hekta.

"Tunataka mpaka kufikia 2025 nchi iwe inajitosheleza kwa ngano ili tuondokane na uagizaji wa ngano hizi kutoka nje ya nchi, kwa sasa tunaagiza asilimia 90 ya ngano zinazotumika nchini tafsiri yake ni kwamba ukinunua maandazi 10 ya ngano basi ujue ni moja pekee ndilo limetengeneza kwa ngano za Tanzania," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema kwa sasa maeneo yanayolengwa zaidi kusambazwa mbegu hizo ni mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma.

Akizungumza baada ya kuzindua uvunaji wa ngano hizo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera aliipongeza TARI kwa utafiti huo ambao alisema utasaidia wakulima kupata mbegu sahihi zilizofanyiwa utafiti wa kutosha.

Aliutaka uongozi wa taasisi hiyo kuendelea kutoa elimu ya kilimo bora cha zao hilo kwa wakulima ili uzalishaji uongezeke kama serikali ilivyoelekeza na wananchi wanatakiwa wahamasishwe kulima zao hilo. Homera alisema katika Mkoa wa Mbeya yapo maeneo mengi yanayofaa kwa kilimo cha ngano na wananchi wa mkoa huo wanajituma kulima wanachohitaji ni elimu ya kilimo bora kutoka kwa wataalamu.

"Endeleeni kuzalisha hizi mbegu hapa tutafanya maarifa ili vichimbwe visima muwe na uwezo wa kuzalisha mbegu muda wote, kwa sasa hakikisha mbegu zinawafikia wakulima mapema ili waendane na msimu wa kilimo," alisema Homera.

Aliwasisitiza wakulima kuchangamkia kilimo cha zao hilo kwa kuwa ni miongoni mwa mazao yenye soko la uhakika la ndani na nje ya nchi.

## Wananchi washauriwa kujiunga ICHF

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WANANCHI wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, wameshauriwa kujiunga na Bima ya Afya iliyoboreshwa (ICHF) ili wapate matibabu kwenye vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya kwa gharama nafuu.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Vincent Anney, wakati alipowatembelea baadhi ya wagonjwa wanaoendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya hiyo ya Makandana kwa kuwaambia bima inasaidia kupunguza gharama za matibabu.

Alisema wananchi wa wilaya hiyo wana uchumi mzuri ambao wanaweza wakautumia kuchangia mfuko huo wa Bima ya afya kwa Sh. 30,000 kwa mwaka kiwango ambacho alisema kitawasaidia wao na familia zao kutibiwa.

"Jiungeni na Bima inasaidia sana kwenye matibabu, magonjwa huwa hayapigi hodi kwa hiyo huwezi ukajua kwamba utaugua lini, unaweza ukaugua siku ambayo huna hela, lakini ukiwa na bima unatibiwa bila matatizo," alisema Dk. Anney.

Katika hatua nyingine Dk. Anney alisema serikali inaendelea kuboresha hospitali hiyo kwa kuleta Sh. bilioni moja kwa ajili ya ukarabati wa baadhi ya majengo yaliyochakaa.

Vilevile, aliweka jiwe la msingi kwenye jengo la mama na mtoto katika hospitali hiyo ambalo limejengwa kwa gharama ya Sh. milioni 481 na lina jumla ya vyumba 42.

# Serikali yatoa mamilioni kukarabati chuo cha kilimo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imetoa zaidi ya Sh. milioni 495.7 kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Chuo cha Kilimo Uyole (MATI-Uyole) cha jijini Mbeya ili kukiwezesha chuo hicho kuwa na uwezo wa kuongeza udahili wa wanafunzi.

Majengo yanayokarabatiwa ni mabweni mawili yenye jumla ya vyumba 128 ambavyo kati yake 76 ni vya wavulana na 52 ni vya wasichana huku pia jengo la utawala likikarabatiwa kwa kufumuliwa paa na kuezekwa upya.

Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Sebastian Mosha, alisema walipatiwa fedha hizo Juni 11, mwaka huu na kuanza kukarabati majengo hayo Juni 22 na wanatarajia kukamilisha mwishoni mwa mwezi ili yaanze kutumika chuo kitakapofunguliwa.

Alisema fedha hizo ni za awamu ya kwanza na waliahidiwa kupatiwa zingine kwa ajili ya kukarabati majengo mengine ambayo yamechakaa kutokana na kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu.

"Tunaishukuru serikali kwa kutupatia fedha hizi na naahidi kwamba tutajitahidi kuhakikisha zinatumika kwa kazi iliyokusudiwa, lakini tunaomba tutakapoomba zingine tupatiwe," alisema Dk. Mosha.

Alisema mabweni hayo yana uwezo wa kuchukua wanafunzi zaidi ya 200 na chuo kina uwezo wa kudahili wanafunzi 500 kwa sasa huku wakiwa na mipango ya kuongeza udahili.

Mhandisi wa Chuo hicho, Abbas Pembe, ambaye ndiye anayesimamia ukarabati wa majengo hayo, alisema mpaka sasa ukarabati umefikia asilimia 70 na maeneo yaliyobakia yatakamilika kabla ya Septemba 22, mwaka huu.

Alisema ili kuhakikisha majengo hayo yanakarabatiwa vizuri, zimeundwa kamati nne za kusimamia ikiwamo ya Kamati ya ununuzi ambayo ndiyo inayoshughulikia ununuzi na ukarabati huo unafanywa kwa mfumo wa akaunti ya dharura (Force Account).

Alisema mabweni ya wanafunzi walianzia kukarabati ndani kwa ni ghorofa, lakini jengo la utawala lilianza kukarabatiwa juu kwa kuezua paa na kuanza upya kuezeka.

Alisema jengo la utawala lilitengewa Sh. milioni 95 na mabweni ya wanafunzi yametengewa Sh. milioni 200 kila moja na kusema fedha hizo zitatosha.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliuagiza uongozi wa chuo hicho kuhakikisha ukarabati wa majengo hayo unakamilika kabla ya Septemba 30, mwaka huu na baada ya hapo atakwenda kuyakagua ili hatua zichukuliwe kwa watakaokuwa wamezembea.

Alisema ataenda kukagua jengo hilo akiwa ameambatana na vyombo vya dola na watakaokuwa wamezembea watakamatwa na kupelekwa mahabusu ili wachukuliwe hatua kali zaidi za kisheria.

Alisema serikali ilipeleka fedha hizo ili chuo hicho kikarabatiwe na kiwe na uwezo mkubwa wa kuzalisha maofisa kilimo ambao watajaza nafasi zilizowazi kwenye vijiji, kata na hata kwenye halmashauri.

"Kwenye mfumo huu wa Force account kuna upigaji sana, sasa epukeni sana kufanya ubadhilifu kwenye fedha za serikali, nitakuja kufuatilia jengo hili mwishoni mwa mwezi nikiwa na polisi," alisema Homera.

Aliutaka uongozi wa chuo hicho kuongeza vitanda kwenye kila chumba ili waongeze udahili wa wanafunzi pamoja na kuhakikisha wanafunzi wanakaa kwenye mazingira mazuri.





# Rais Mwinyi akerwa wananchi kudhulumiwa mashamba karafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuna dhuluma kubwa ya ardhi kisiwani Pemba, ambapo baadhi ya wananchi wamenyang'anywa mashamba yao ikiwamo ya karafuu. Aliyasema hayo juzi wakati wa majumuisho ya ziara yake kisiwani Pemba wakati akizungumza na watendaji katika ukumbi wa kiwanja cha kufurahishia watoto Tibirinzi Pemba.

Dk. Mwinyi alisema lazima kukomesha dhuluma hiyo kwa sababu kuna watu wamenyang'anywa mashamba yao ya karafuu na baadhi ya watendaji wa serikali, hivyo aliwaagiza wakuu wa mikoa kushughulikia kesi zinazotokana na dhuluma kwa wananchi.

"Tumeapa kutenda haki, hatuwezi kuachia watu kudhulumiwa, wengine wamekwenda mpaka mahakamani kudai haki yao na wameshinda kesi, lakini hawajapewa haki yao," alisema Dk. Mwinyi.

Alieleza kuwa kama serikali ipo haitokubali hayo kuendelea kufanyika, na kuwataka viongozi wakuu kuchukua hatua zinazostahiki ili haki itendeke.

Aidha aliwataka watendaji wenye tabia ya kuwadhulumu wananchi mashamba yao ya karafuu kuacha mara moja na kuhakikisha wananchi wanapata haki zao.

"Hata kama wewe chombo cha ulinzi na usalama umemkamata mtu ana mali yake na unahisi amefanya kosa mhukumu kwa kosa lake, lakini mali yake muachie mwenyewe na sio kumpora," alisema Dk. Mwinyi.

Aidha, alitaka uzalishaji wa karafuu uongezeka kisiwani Pemba ili zao hilo liongezeke na kutoridhika na kiwango cha uzalishaji kiliopo sasa.

Alisema lazima kuifanya karafuu ya Zanzibar kuwa na hadhi yake kwa sababu ni karafuu bora duniani, hivyo lazima kulinda ubora huo.

Dk. Mwinyi aliagiza kuwa kwa wale ambao wazazi waliokuwa wakimiliki mashamba ya kilimo ya heka tatu yaliyotolewa na serikali na wazazi hao wameshafariki dunia, mashamba hayo wapewe watoto wao kuyaendeleza na sio kupewa watu wengine. "Naliagiza Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kutoa miche ya karafuu kwa wananchi ili kuongeza uzalishaji wa zao la karafuu kwa sababu zao hili ni muhimu sana hasa kwa wananchi wa Pemba," alisema.

Alieleza kuwa licha ya dunia kukabiliwa na janga la ugonjwa wa corona, lakini bei ya zao hilo haijateremka kwa kuwa kilo moja ya karafuu kwa daraja la kwanza inauzwa Sh. 14,000.

Akizungumzia kuhusu rasilimali ya mafuta na gesi asilia, Dk. Mwinyi alisema Zanzibar ina utajiri mkubwa wa rasilimali hiyo, hivyo ikifanyiwa kazi itaondokana na umaskini.

Alisema Zanzibar ina mafuta na gesi nyingi, na kwamba kampuni ya Ras Gas wameshagundua kiasi cha gesi kiliopo ni trilioni 3.2. "Ninapozungumzia uchumi wa bluu namaanisha mambo matano ikiwamo utalii, uvuvi, ukulima wa mwani, bandari, mafuta na gesi...najua kuna kejeli nyingi, lakini ishallah Mungu atupe uhai haya yote yatafanikiwa," alisema Dk. Mwinyi.



Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza juzi na watendaji wa serikali wa mikoa miwili ya Kaskazini na Kusini Pemba katika mkutano wake wa majumuisho ya ziara katika mikoa hiyo, uliofanyika ukumbi wa Kiwanja cha Watoto Tibirinzi Chakechake Pemba. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Sababu kupaa bei ya saruji yaanikwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BEI ya saruji visiwani Zanzibar imepanda kutoka Sh. 14,000 hadi Sh. 18,000 kwa saruji ya Oman, kutokana na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji wa bidhaa hiyo kulikotokana na baa la corona duniani.

Waziri wa Biashara na Viwanda, Omar Said Shabani, aliwataka wafanyabiashara visiwani Zanzibar kufuata bei elekezi iliyotolewa na serikali ili wananchi kumudu gharama za bidhaa hiyo.

Akizungumza jana baada ya kufanya ziara katika Bandari ya Malindi Mjini Unguja kuangalia uingizaji wa saruji, alisema kwa sasa bidhaa hiyo ipo ya kutosha kufuatia kuingizwa nchini tani 36 za saruji kutoka Oman.

Alisema serikali imetoa bei elekezi ya bidhaa hiyo kwa wafanyabiashara wa jumla na rejareja ambayo wanatakiwa kuifuata na atakaekiuka kwa kuongeza bei kinyume cha iliyotangazwa na serikali atachukuliwa hatua za kisheria.

Saruji ambayo inazalishwa Tanzania kwa sasa mfuko mmoja unauzwa kwa Sh.16,000 ambapo awali ilikuwa ikiuzwa Sh. 12,000 na saruji kutoka Oman kwa sasa inauzwa Sh. 18,000 kutoka Sh. 14,0000 za awali.

Serikali ya Zanzibar imeamua kutangaza bei elekezi ya bidhaa hiyo kutokana na wafanyabiashara kuuza saruji mfuko mmoja kwa Sh. 20,000, hali ambayo ilizua malalamiko mengi kutoka kwa wananchi.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, mafundi ujenzi, walisema ajira za ujenzi zimepungua kutokana na baadhi ya wananchi kusitisha ujenzi wa nyumba zao.

Juma Makame, alisema baadhi ya wateja wake wamesitisha ujenzi kutokana na kupanda ghafla kwa bei ya saruji, hali ambayo imesababisha kipato chake kupungua.

"Wateja wangu ninaowajengea ni wale wanyonge, lakini kutokana na saruji kupanda bei, baadhi yao wamesitisha ujenzi wakiwa na matumaini kuwa bei ya saruji itarudi kama kama ya awali," alisema.

Mwishoni mwa wiki hii Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi. aliwataka wafanyabiashara kuacha kutopandisha bei za bidhaa kwa kisingizio cha ugonjwa wa corona.

"Nafahamu kuwa ugonjwa wa corona umepelekea baadhi ya bidhaa ikiwamo saruji usafirishaji wake kuwa mkubwa, lakini niwaombe wafanyabiashara kuwahurumia wananchi," alisema Dk. Mwinyi.

# Hemed aagiza matumizi ya baiskeli Mji Mkongwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameyataka mabaraza na jumuiya za uhifadhi na uendelezaji Mji Mkongwe kuendelea kutoa hamasa kwa wakazi na wageni wanaotembelea mji huo ili kujenga utamaduni wa kutumia usafiri wa baiskeli badala ya vyombo vya moto.

Lengo la agizo la Makamu wa Pili wa Rais ni kuendelea kuhifadhi mji huo.

Hemed alieleza hayo jana katika mapokezi maalum ya matembezi ya usafiri wa baiskeli yaliyofanyika katika bustani ya Forodhani Mjini Zanzibar, ambapo alishiriki kwa kuendesha baiskeli kuanzia ukumbi wa Sheikh Idriss Abdulwakil na kumalizia katika eneo la bustani ya Forodhani.

Alieleza kuwa kampeni ya kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya matumizi ya baiskeli katika eneo la Mji Mkongwe itasaidia kwa kiasi kikubwa kuhifadhi na kuendeleza mji huo na kupunguza athari mbalimbali za kimazingira.

Alisema kitendo cha utumiaji wa usafiri wa baiskeli mbali na kupunguza athari katika mitaa ya mji huo wa kale, pia kutasaidia kuimarisha afya za watu ikiwa utumiaji wa usafiri wa baiskeli kuwa sehemu mojawapo ya kufanya mazoezi.

Makamu wa Pili wa Rais alisema katika kukabiliana na changamoto hiyo, serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kupunguza uingiaji holela wa vyombo vya moto wa kutunga sheria na kanuni za usafiri zinazodhibiti uingiaji wa vyombo hivyo pamoja na kuhamasisha matumizi ya usafiri mbadala.

"Tumekuwa tukihamasisha wananchi kutumia usafiri mbadala yakiwamo matumizi ya usafiri baiskeli ili kukabiliana na changamoto," alisema Makamu wa Pili wa Rais.

Hemed alisema katika kukabiliana na changamoto, serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa kuweka miundombinu rafiki ya kuwawezesha wananchi kutembea kwa miguu na kutumia baiskeli katika mitaa ya Mji Mkongwe.

"Sambamba na yote serikali imekuwa ikishirikiana na jumuiya za kiraia za ndani na nje ya nchi katika kuhakikisha kuwa tunapunguza matumizi ya vyombo vya moto ili kuunusuru mji wetu usiendelee kuharibika," alisema.

Naye Kaimu Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Suleiman Masoud Makame, ambaye ni Waziri wa Maji Nishati na Madini, alisema kuna umuhimu kwa viongozi kuweka utaratibu maalum wa kutembea kwa baiskeli ili kutoa hamasa kwa wananchi kutumia usafiri huo.

Aidha, alisema kutembea kwa baiskeli katika Jiji la Zanzibar ni ishara tosha ya kuwapo kwa amani na utulivu ndani ya Zanzibar, ambapo jambo hilo linawapa fursa wageni kuja kwa wingi kuitembelea Zanzibar.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Tamasha la Nyama choma ambaye ni Katibu wa CCM Wilaya ya Mjini, Abdulrahim Hamid, alisema kufanyika kwa matembezi hayo kunalenga kuunga mkono jitihada za Rais za kuinua Mji Mkongwe na kuimarisha utalii kupitia uchumi wa bluu.

## HABARI KITAIFA

# Wajasiriamali waeleza fursa waliyoipata kuuza bidhaa nje

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

WAJASIRIAMALI wengi nchini wameanza kuuza bidhaa zao nje ya nchi baada ya kupewa alama ya ubora wa bidhaa zao.

Wajasiriamali hao walitoa ushuhuda huo mwishoni mwa wiki, wakati wa maonyesho ya 18 ya wahandisi yanayoendelea katika ukumbi wa mikutano wa Jakaya Mrisho Kikwete, jijini Dodoma.

Anna John, mkazi wa Dar es Salaam, alisema kabla ya kupata alama ya ubora kila alipokuwa akipeleka bidhaa zake kwenye soko, alikuwa anaulizwa kama ina alama ya ubora ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Alisema hicho kilikuwa kikwazo kikubwa kwake, lakini tangu amepata alama hiyo anauza bidhaa zake hata kwenye nchi jirani.

"Kwa hiyo nawasihi wajasiriamali wezangu kujitokeza TBS kuthibitisha ubora wa bidhaa kwa sababu ni bure, hivyo hawana sababu ya kubaki nyuma, waje kwetu waone mafanikio tuliyopata," alisema.

Mwingine Ibrahim Jengo alisema alama ya ubora imemwezesha yeye na wajasiriamali wengi rafiki zake kuuza bidhaa zao kwenye nchi za Afrika Mashariki bila vikwazo.

Alitoa wito kwa wajasiriamali wenzake kwenda TBS kupata nembo ya ubora itakayowawezesha kuuza bidhaa zao nje ya mipaka ya Tanzania.

Wakati huo huo, wahandisi wameshauriwa kushiriki mchakato wa uandaaji viwango ili kuleta uelewa wa pamoja kuhusu viwango vya kitaifa vinavyoandaliwa kwa bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini.

Wito huo ulitolewa na Mkaguzi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Domisiano Rutahala kwenye maonyesho hayo.

Alisema wahandisi ni sehemu muhimu sana katika uzalishaji uzalishaji wa bidhaa nchini, hivyo ushiriki wao katika mchakato wa uandaaji viwango kwa kutoa maoni kutaleta tija kwa shirika na taifa kwa ujumla.

Rutahala alisema mchakato wa uandaaji viwango uhusisha wadau mbalimbali katika sekta husika ambao hukutana na kuandaa viwango vya kitaifa na baadaye viwango vilivyoandaliwa huwekwa kwenye tovuti ya TBS kwa ajili ya kupata maoni.

Akizungumzia faida ya viwango, Rutahala alisema ni kuleta usawa katika uwanja wa biashara, kurahisisha biashara baina ya nchi na nchi na hulinda afya na usalama wa watumiaji wa bidhaa.

Kwa upande wake, Ofisa Masoko TBS, Rhoda Mayugu, alisema maonyesho hayo yametumika kama sehemu ya kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya TBS, ambayo ni pamoja na kuthibitisha ubora wa bidhaa, usajili wa majengo ya chakula na vipodozi, usajili wa chakula na vipodozi na msaada wa kiufundi kwa wasafirishaji wa bidhaa nje ya nchi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Hisham Hendi, akizungumza na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Dk. Tulia Ackson, alipotembelea ofisi za kampuni hiyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau washauri elimu itolewe kutokomeza udumavu

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

WADAU wa lishe bora katika Manispaa ya Morogoro wameshauriwa kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa jamii ili kutokomeza udumavu kwa watoto na kuwa na jamii yenye afya bora itakayowezesha kuleta maendeleo kwa taifa.

Kauli hiyo imetolewa na Ofisa Tarafa wa Manispaa hiyo, Winfred Kipako, wakati wa uzinduzi wa Siku ya Lishe na Afya kwa Kata ya Mwembesongo, kwenye manispaa hiyo.

Alisema Manispaa ya Morogoro haina shida ya vyakula, na sio sahihi kwa wananchi wa kata hiyo na nyinginezo kukabiliwa na tatizo la udumavu wa watoto.

"Lazima tubadilike ili kuondokana na hii hali kwenye kata ya Mwembesongo, watoto wetu waendelee na udumavu wakati tunalima matunda ya kutosha, mboga za majani za kutosha, nafaka na vyakula vya kila aina vyenye virutubishi vya mwili," alisema Kipako.

Kipako alisema, suala la lishe limekuwa ni tatizo mtambuka katika taifa na kwamba ni wajibu kwa wadau wote katika manispaa hiyo na Kata ya Mwembesongo kupambana na suala la lishe.

Naye Mtendaji wa Kata ya Mwembesongo, Amina Said, alitaja baadhi ya sababu za hali ya udumavu kwa watoto ni baadhi ya wazazi kushindwa kuzingatia muda kuwalisha watoto vyakula vinavyohitajika vyenye virutubishi ipasavyo. Pia lishe duni, wazazi kutokuwa na elimu ya ulaji wa chakula cha kutosha na chenye mchanganyiko wa viini lishe kwenye jamii zao.

Alisema kutokana na changamoto hiyo, Kata ya Mwembesongo inatarajia kuweka mikakati mbalimbali ya kupambana na hali ya utapiamlo na udumavu kwa watoto wenye chini ya miaka mitano.

Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa elimu ya nadharia na vitendo kwa jamii kuhakikisha kwamba ulaji wa kiwango cha juu cha virutubishi unafanyika na kuzingatia unyonyeshaji katika siku 1,000 za mtoto unafuatwa.

Kwa upande wake, mkazi wa kata hiyo, Juma Abdallah, aliupongeza uongozi wa Kata ya Mwembesongo kwa kuifanya siku ya lishe katika kata hiyo na wananchi kunufaika kwa kupata elimu kubwa ambayo na wao wataifikisha kwa wananchi wengine ili kila mtu anufaike kwa lengo la kuwa na jamii yenye afya bora kwa maendeleo ya taifa.

# Washindi wa shindano Vodacom kuvuna bil. 4/-

**Na Christina Mwakangale**

VODACOM Tanzania kupitia shindano la Tusua Mapene imetoa jumla ya Sh. bilioni nne ikiwa ni zawadi kwa washindi, ambao hupatikana kila siku, wiki na mwezi.

Zawadi za mashindano hayo huanzia Sh. 15,000, Sh. milioni 20 hadi 100 na mwezi wa saba mwaka huu, shindano lilitangaza ushindi mkubwa kabisa katika historia yake ya miaka minne, kwa mshindi kujinyakulia zawadi ya Sh. milioni 180.

Celestine Kilemezi kutoka Musoma mkoani Mara, aliyeshinda Sh. milioni 28, alisema ushindi huo umemsaidia kujenga nyumba, kununua gari na kiwanja.

"Nilipata mshangao mkubwa mjukuu wangu aliponiletea simu saa moja usiku na nikaambiwa kwenye kipindi cha televisheni kuwa nimeshinda!"

Celestine alieleza kuwa hakukuwa na matatizo yoyote kupokea ushindi wake, alipigiwa simu na maofisa wa Vodacom waliopanga siku ya kukutana na kukabidhiwa hundi yake.

Wakati wa makabidhiano, Mkurugenzi wa VAS wa Vodacom Tanzania, Nguvu Kamando alisema: Lengo la Tusua Mapene ni kuwawezesha Watanzania kiuchumi. Nawahimiza wateja wetu kushiriki katika shindano hili linaloendelea kwa sababu kwa kufanya hivyo unajipatia nafasi ya ushindi mkubwa."

Mwanzoni mwa mwaka jana, Eveneth Rutiyomba ambaye ni mkazi wa Dar es Salaam alishinda Sh. milioni 150.

"Hii ni ndoto kwangu, sikutegemea hata siku moja kuwa ningeshika pesa nyingi kiasi hiki maishani mwangu, lakini leo hii niko hapa na maisha yangu yamebadilika kabisa."

Mshindi mwingine, Marko Kilungala, alishinda Sh. milioni 80 na alitumia pesa hizo kununua kiwanja na amejenga nyumba anayosihi kwa sasa.

Pia mshindi mwingine, Jackson A. Mwankemwa mwenye umri wa miaka 51, mkulima kutoka Kijiji cha Msasani, wilayani Rungwe mkoani Mbeya alishinda Sh. milioni 200. Mashindano ya Tusua Mapene yameingia awamu nyingine mshindi mkuu mwingine atapatikana na maisha yake kubadilika milele.

HABARI KIMATAIFA

# Taliban yalisotea jimbo la Panjshir

**Kabul,** AFGHANISTAN

KUNDI la Taliban na vikosi vya wapiganaji pinzani wamekabiliana mwishoni mwa wiki, kudhibiti jimbo la Panjshir, Kaskazini mwa mji wa Kabul, likiwa ni eneo la mwisho Afghanistan, kutwaliwa na Taliban.

Pande zote mbili zimedai kuwa zinalidhibiti eneo la juu la bonde la Panjshir, ingawa hakuna upande wowote uliotoa ushahidi wa hilo.

Kundi la Taliban, ambalo limefanikiwa kuchukua udhibiti wa karibu nchi nzima wakati vikosi vya kigeni vilipokusanya virago na kuondoka Afghanistan, halikuweza kulitawala eneo la Panjshir lilipokuwa likiiongoza Afghanistan kuanzia mwaka 1996 hadi 2001.

Msemaji wa Taliban, Bilal Karimi, aliarifu kuwa Wilaya za Khinj na Unabah, zimekamatwa, hatua iliyowezesha wapiganaji wa Taliban kuchukua udhibiti wa wilaya nne kati ya saba za jimbo la Panjshir.

"Wapiganaji wa Taliban wanasonga mbele kuelekea katikati mwa jimbo hilo," aliandika Karimi kwenye ukurasa wake wa Twitter.

Hata hivyo kundi la wapiganaji wa National Resistance Front of Afghanistan wanaomtii kiongozi wa eneo la Panjshir Ahmad Massoud, lilisema kuwa limewazingira maelfu ya magaidi kwenye mji wa Khawak na kwamba wapiganaji wa Taliban wameyatelekeza magari na vifaa vingine kwenye eneo la Dashte Rewak.

Msemaji wa kundi hilo pinzani Fahim Dashti amezungumzia kile amekiita mapambano makali kuwa yanaendelea.

Kupitia ujumbe kwenye ukurasa wa Facebook, Massoud alisisitiza kuwa Panjshir inaendelea kusimama imara.

Msemaji huyo pia amewasifu wanawake waliondamana mjini Herat kudai haki zao akisema wameonesha Waafghani hawajakata tamaa kudai haki na hawaogopi vitisho.

Wakati hayo yakijiri Mkuu wa Jeshi la Marekani, Jenerali Mark Milley, alizungumzia uwepo wa hali tete nchini Afghanistan.

"Fikra zangu za kijeshi ni kwamba hali iliyopo inaweza kuzidi makali na kuwa vita vya wenyewe kwa wenyewe. Sifahamu iwapo Taliban wataweza kuchukua udhibiti kamili na kutawala" amesema Jenerali Milley.

Akizungumza na kituo cha televisheni cha Fox News kutoka uwanja wa ndege wa jeshi wa Ramstein nchini Ujerumani, Milley amesema iwapo Taliban haitomudu kudhibiti hali ya mambo hilo litachochea kushamiri tena kwa makundi ya itikadi kali ikiwamo Al Qaeda au kundi linalojiita Dola la Kiislamu au makundi mengine "kigaidi" miaka mitatu inayokuja.

Wakati mapambano yakiendelea huko Panjshir, mjini Kabul shamrashamra zililipuka baada ya kuzagaa kwa taarifa kuwa Taliban wamelikamata jimbo la Panjshir.

Mashirika ya habari ya kimataifa yameripoti kuwa risasi zilizofyatuliwa kusherehekea taarifa hizo zimewaua watu 17 na kuwajeruhi zaidi ya watu 40.

**DW**



# Wananchi Sao Tome na Principe wapiga kura

**São Tomé,** SAO TOME NA PRINCIPE

WANANCHI wa Sao Tome na Principe wamepiga kura jana katika uchaguzi wa duru ya pili, ukiwa ni mchuano kati ya aliyekuwa Waziri wa Miundombinu Carlos Vila Nova, aliyeshinda katika duru ya kwanza na Waziri Mkuu wa zamani Guilherme Posser da Costa.

Duru ya kwanza ya uchaguzi ilifanyika Julai kwenye visiwa inayotazamwa kama mfano wa nchi inayofuata demokrasia inayozingatia sheria katika eneo la Afrika ya Kati.

Nchi ya Sao Tome inaangaliwa kama mfano pia ni nchi yenye maslahi kwa sekta ya mafuta zikishuhudiwa kampuni za uchimbaji mafuta zilizoweka matumaini ya kupata hifadhi ya mafuta nchini humo. Wananchi 123,000 wenye vigezo vya kupiga kura, waliojiandikisha watamchagua rais mpya atakayemrithi Evaristo Carvalho, mwenye umri wa miaka 79. Hakugombea muhula mwingine wa miaka mitano katika nafasi hiyo ambayo kimsingi haina mamlaka makubwa.

Duru hii ya pili ya uchaguzi wa rais ilicheleweshwa wakati mgombea wa nafasi ya tatu, Delfim Neves alipodai umefanyika udanganyifu na kutaka kura na zihesabiwe upya.

Duru hii ya pili mwanzoni ilipangwa kufanyika Agosti 8, mwaka huu, ukaahirishwa hadi Agosti 29 na kisha kucheleweshwa tena baada ya malalamiko ya udanganyifu yaliyotolewa na Delfim Neves.

Mahakama ya Katiba, ilikataa ombi lake. Kuna vituo 262 vya kupiga kura katika nchi nzima ambayo ni koloni la zamani la Ureno katika ghuba ya Guinea.

Katika kipindi cha miongo miwili iliyopita kwa mujibu wa benki ya dunia, ukuaji katika nchi hiyo umechochewa zaidi na bajeti ya matumizi ya serikali ikisaidiwa na msaada kutoka nje na mikopo, iliyochukuliwa na serikali pamoja na kilimo, utalii na uwekezaji wa kigeni katika sekta ya uchimbaji mafuta.

Sao Tome na Principe iliingia kwenye mfumo wa vyama vingi 1991 baada ya miaka 15 ya utawala wa chama kimoja wa serikali ya Kimaxist.

Carlos Vila Nova ni kiongozi wa chama cha upinzani cha siasa za wastani za mrengo wa kulia cha Independent Democratic Action ADI na aliongoza katika matokeo ya duru ya kwanza Julai 18, mwaka huu kwa kupata asilimia 39.5 ya kura.

Ni mfanyabiashara mwenye umri wa miaka 62 na alikuwa waziri wa miundombinu lakini ni miongoni mwa watu ambao hawajulikani sana na umma.

Mpinzani wake wa karibu Gulherme Posser da Costa mwenye umri wa miaka 68 anatokea chama cha siasa za wastani za mrengo wa kushoto, kinachojulikana kama chama cha ukombozi wa Sao Tome na Principe MLSTP, alipata asilimia 20.7 katika duru ya kwanza.

Chama chake ndicho kinachoongoza muungano tawala katika bunge la nchi hiyo.

Rais hana madaraka makubwa nchini humo, bali jukumu lake ni la usuluhishi katika mivutano ya kisiasa, madaraka makubwa yako kwa waziri mkuu ambaye hivi sasa ni Jorge Lopes Bom Jesus kutoka Chama cha MLSTP kilichoshinda uchaguzi mwaka 2018.

**DW**



Waafghanistan ambao wanajihusisha na shughuli ya kubadilisha fedha za kigeni wakisubiri wateja, eneo la mji wa Kabul, nchini Afghanistan, juzi. Soko kwa ajili ya kubadilisha fedha limefunguliwa tena Jumamosi iliyopita baada ya Taliban kuchukua mamlaka huku benki nchini humo zikikumbwa na anguko la kifedha. **PICHA: XINHUA**

# Malori 600 ya misaada yawasili Tigray

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

ZAIDI ya malori 600 ya misaada ya kibinadamu yaliingia katika mkoa wa Tigray, kulikokuwa na mamilioni ya watu wenye hatari ya kufa njaa, kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, (UN).

Tangu wiki iliyopita, mamlaka zimefanya juhudi kuratibu na kuwezesha kusafirishwa kwa misaada ya kibinadamu kwenda Tigray, wizara ya amani ya Ethiopia ilisema.

Karibu malori 500 yaliwasili Tigray tangu wiki iliyopita, ikiwa ni pamoja na malori 152 katika siku mbili zilizopita, wizara ilisema katika taarifa iliyochapishwa kwenye Twitter.

Inakadiriwa watu milioni 5.2, sawa na asilimia 90 ya wakazi wa Tigray, wanaohitaji msaada wa haraka 400,000 ni ambao tayari wanakabiliwa na baa la njaa.

Siku ya Alhamisi, Kaimu Mratibu wa misaada ya kibinadamu kwa Ethiopia, Grant Leaity, alionya kwamba hali hiyo itazidi kuwa mbaya.

Mamilioni ya watu wako katika hatari ya kufa na njaa, wakiwamo watu milioni 1.7 katika mikoa ya Afar na Amhara, aliongeza: Akiba ya misaada ya kibinadamu, pesa taslimu na mafuta ni ndogo sana au imepungua kabisa".

Mamlaka ya Ethiopia na waasi wa Tigray wamekuwa wakishtumiana kwa kuzuia misafara ya malori ya misaada ya kibinadamu yanayojaribu kuingia katika jimbo la Tigray.


**RFI**







# SANCHO AONDOLEWA KIKOSI CHA ENGLAND



**LONDON,** England

MCHEZAJI wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, ameondolewa kwenye kikosi hicho baada ya kupata jeraha dogo.

England iliinyuka Hungary mabao 4-0 kule Budapest Alhamisi na kukamilisha ushindi wa nne katika michezo minne ya kufuzu Kombe la Dunia nchini Qatar 2022.

Winga huyo sasa hajahusishwa kwenye kikosi kuelekea mchezo wao dhidi ya Andorra na Poland pia.

England ilithibitisha Jumamosi kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amerejea kwenye klabu yake, lakini anatarajiwa kucheza katika mchezo wa 'Mashetani Wekundu' hao dhidi ya Newcatle United Jumamosi ya Septemba 11.

Katika mchezo huo utakaopigwa kwenye dimba la Old Trafford, unaweza kumhusisha pia Cristiano Ronaldo akicheza tena kwa United tangu alipoondoka mwaka 2009 na kurejea wakati wa dirisha la usajili.

Kocha Gareth Southgate ambaye timu yake jana Jumapili ilikabiliana na Andora na Poland Jumatano, itamkosa pia Dominic Calvert-Lewin ambaye anakabiliwa na jeraha la paja.



## MADRID NA MIKATABA YA MBAPPE MKONONI

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid inaripotiwa kuwa iliandaa mikataba mingi kwa kipindi cha mwezi uliopita ili kumvutia Kylian Mbappe.

Mikataba inayoripotiwa kuandaliwa ilifikia saba kwa kikosi hicho kwenye harakati zake za kuwania saini ya nyota huyo wa Ufaransa.

Real Madrid walikuwa tayari kulipa euro milioni 220 kabla ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho la msimu wa majira ya joto ili kumnasa staa huyu wa Paris Saint Germain.

Hata hivyo, PSG wao hawakutaka kujibu ofa ya Real Madrid kumruhusu Mbappe aondoke, na mpaka sasa wapo kwenye hatari ya kumpoteza bure mwaka ujao, ikiwa hataongeza mkataba kusalia PSG.

Kwa mujibu wa vyanzo kadhaa, ikiwamo ABC, maofisa wa klabu hiyo ya LaLiga, walifanyia kazi maboresho ya mikataba mara kadhaa katika kuweka masharti ambayo yanaonekana kuvutia zaidi kwa kipaumbele chao cha usajili.

Mkataba wowote ambao Mbappe angesaini na Real Madrid unatazamiwa kuwa wa angalau miaka sita, huku staa huyu mwenye miaka 22, akitarajiwa kuvuta euro milioni 30 kwa msimu, na uwakilishi wake ukinufaika na bonasi ya euro milioni 60.

Kwa kuwa bado staa huyu mpaka sasa hajasaini mkataba mpya na PSG, bila shaka Real Madrid wataanzisha jitihada rasmi za kuiwinda saini yake tena mapema mwakani.

## HABARI MICHEZO

LIVE IN PLAY
BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP
CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA

PAKUA SASA

# NEYMAR AANGUA KICHEKO KUAMBIWA KANENEPA



**RIO DE JANEIRO,** Brazil

NEYMAR aliangua kicheko baada ya mashabiki wa soka kudai kwamba amekuwa mzito kutokana na kukosolewa kuwa hayupo katika umbo zuri la kucheza mpira.

Nyota huyo wa Brazil alicheza dakika zote katika mchezo wa Alhamisi wakati Brazil ikipata ushindi mwembamba dhidi ya Chile katika kuitafuta tiketi ya kucheza Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar.

Vyombo vya habari vya Ufaransa vilisema kwamba, hayupo katika umbo zuri baada ya ushindi wa PSG dhidi ya Reims wikendi iliyopita, hali iliyomsukuma kujibu baada ya kucheza akiwa na Brazil.

Neymar aliposti katika Instagram yake, akisema wakati wa mechi ya Chile: "Tumecheza vizuri? Hapana! Tumeshinda? Ndiyo!"

Kisha akaelezea kukosolewa kwake kwa uzito alionao: "Kipimo cha fulana kilikuwa saizi kubwa, nipo katika uzito wangu, mchezo ujao."

# EMERSON AUMIZWA KUUZWA NA BARCA



**LONDON,** England

LICHA ya kusajiliwa Barcelona msimu huu wa majira ya joto kutoka Real Betis, Emerson Royal, aliachana na 'Blaugrana' hao siku ya mwisho na kujiunga na Tottenham Hotspur.

Beki huyo wa kulia mwenye umri wa miaka 22, ameelezea kutofurahishwa kwake na jinsi alivyotendewa na timu hiyo kutoka Catalunya na kusisitiza kuwa ndoto yake ilikuwa kujiimarisha katika kikosi cha kwanza cha Barcelona.

Katika mahojiano na Marca, Emerson alielezea kwamba hakutarajia kuondoka klabuni hapo msimu huu wa majira ya joto, lakini alionyesha kwamba analenga kufanikiwa huko Spurs.

"Nilikuwa Betis na ilikuwa wazi kwangu kwamba mwisho wa msimu ningeenda Barcelona. Hii ilikuwa imeainishwa katika mkataba wangu," alisema.

"Ni kweli kwamba nilisikia habari nyingi ambazo zilisema kwamba kulikuwa na klabu zingine huko Hispania na nje ya nchi ambazo zilinipenda, lakini nilijua kwamba mkataba wangu ulisema ningeenda Barcelona. Nilikwenda likizo yangu na ndivyo ilivyotokea niliporudi.

"Kwa kweli ilikuwa ndoto yangu. Nimekuwa nikisema jambo lile lile kwa sababu ilikuwa ndoto yangu tangu nilipokuwa mtoto. Nilitaka kuja kuhisi ni nini kucheza kwa Barcelona. Ilikuwa ndoto yangu. Nilianza kupendana na Barcelona nikimtazama Ronaldinho Gaucho akicheza, kisha akaja (Lionel) Messi, Neymar na (Dani) Alves.

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 06 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2761 | Odds BK 2 vs Egersund IK | 4.73 | 4.15 | 1.56 |
| 16:00 | 1687 | Benin vs DR Congo | 2.53 | 3.01 | 2.72 |
| 16:00 | 5527 | Uganda vs Mali | 3.39 | 2.86 | 2.22 |
| 17:00 | 3471 | Cobresal vs Nublense | 1.99 | 3.30 | 3.45 |
| 19:00 | 1773 | South Africa vs Ghana | 2.07 | 3.00 | 3.58 |
| 19:00 | 2166 | Guinea vs Morocco | 3.82 | 3.09 | 1.96 |
| 19:00 | 2684 | Czech Republic U21 vs Albania U21 | 1.24 | 5.18 | 10.56 |
| 19:00 | 5884 | Os TF vs Lysekloster | 3.15 | 5.00 | 1.84 |
| 19:15 | 1640 | Dalum vs Naesby BK | 2.43 | 3.40 | 2.57 |
| 19:30 | 4641 | Faroe Islands U21 vs France U21 | 16.50 | 8.15 | 1.10 |
| 20:00 | 1347 | Osters IF vs Vasteras SK | 2.13 | 3.25 | 3.55 |
| 20:00 | 3015 | Andorra U21 vs Slovenia U21 | 21.36 | 7.77 | 1.09 |
| 20:00 | 3529 | Osnabruck vs Viktoria Koln | 2.03 | 3.54 | 3.29 |
| 20:00 | 3948 | Deportes Temuco vs Magallanes | 1.91 | 3.24 | 3.82 |
| 20:00 | 4223 | GIF Sundsvall vs Orgryte IS | 1.71 | 3.89 | 4.59 |
| 20:30 | 3919 | SV Rot-Weiss Walldorf vs SC 1929 Waldgirmes | 1.83 | 4.20 | 3.65 |
| 20:30 | 5201 | FC Speyer 09 vs FV Dudenhofen | 4.85 | 4.56 | 1.49 |
| 21:00 | 4316 | Portugal U21 vs Belarus U21 | 1.01 | 14.54 | 67.85 |
| 21:15 | 5855 | Fluminense RJ U20 vs Palmeiras SP U20 | 2.71 | 3.24 | 2.40 |
| 21:45 | 4825 | CS 2 de Mayo vs Atyra FC | 1.84 | 3.68 | 3.58 |
| 22:00 | 1039 | Bolton vs Burton | 2.22 | 3.36 | 3.06 |
| 22:00 | 1990 | Modena vs AC Reggiana | 2.16 | 3.20 | 3.50 |
| 22:00 | 2576 | Huesca vs Real Oviedo | 1.72 | 3.35 | 5.12 |
| 22:00 | 5372 | Ivory Coast vs Cameroon | 2.26 | 2.86 | 3.30 |
| 22:00 | 5392 | Red Star vs Orleans | 2.31 | 2.89 | 3.28 |
| 22:00 | 5765 | Tigres FC (COL) vs Real Santander | 2.18 | 3.03 | 3.27 |
| 22:00 | 5879 | Deportivo Capiata vs Sportivo Trinidense | 1.64 | 4.26 | 3.97 |
| 23:00 | 1827 | FC Aguablanca vs Valledupar FC | 2.54 | 2.83 | 2.88 |
| 23:00 | 3768 | Coquimbo vs Cobreloa | 1.96 | 3.10 | 3.83 |

### JUMANNE - 07 - SEPTEMBA 2021

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 1864 | Rionegro Aguilas vs Deportivo Pereira | 1.96 | 3.10 | 3.83 |
| 00:00 | 2216 | Estudiantes LP vs Argentinos Juniors | 2.26 | 2.86 | 3.30 |
| 01:00 | 4156 | Toluca W vs Necaxa W | 1.32 | 4.84 | 7.75 |
| 02:00 | 1529 | Figueirense vs Ituano SP | 2.89 | 2.74 | 2.60 |
| 02:00 | 1900 | Union San Felipe vs San Luis Quillota | 2.08 | 3.14 | 3.38 |
| 02:00 | 2448 | Arturo Fernandez Vial vs San Marcos | 2.24 | 2.99 | 3.18 |
| 02:00 | 3950 | Deportes Tolima vs Envigado FC | 1.52 | 3.72 | 5.99 |
| 02:00 | 4132 | Rangers vs Univ de Concepcion | 2.13 | 3.15 | 3.25 |
| 02:00 | 4178 | Univ de Chile vs La Serena | 1.67 | 3.63 | 4.55 |
| 02:00 | 4889 | Avai vs Vasco da Gama | 2.51 | 2.85 | 2.90 |
| 02:15 | 3938 | Velez Sarsfield vs Union Santa Fe | 1.84 | 3.34 | 3.97 |
| 03:00 | 1498 | Pachucha W vs Monterrey W | 3.87 | 3.82 | 1.74 |
| 04:05 | 2288 | Millonarios FC vs Patriotas FC | 1.31 | 4.55 | 9.10 |
| 05:00 | 1735 | Club Tijuana W vs Leon W | 1.75 | 3.58 | 4.07 |
| 13:00 | 1365 | Matsumoto Yamaga vs Kyoto Sanga | 4.45 | 3.24 | 1.78 |
| 14:00 | 4062 | South Korea vs Lebanon | 1.14 | 6.38 | 16.42 |
| 15:00 | 4042 | Vietnam vs Australia | 13.52 | 5.80 | 1.18 |
| 16:00 | 1964 | Tanzania vs Madagascar | 2.26 | 2.95 | 3.19 |
| 16:00 | 4546 | Zambia vs Tunisia | 3.00 | 2.81 | 2.47 |
| 16:00 | 4970 | Malawi vs Mozambique | 2.90 | 2.85 | 2.75 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH ATAKA MZIGO MREFU KUSAINI LIVER

Aiambia iweke mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki mezani kama inataka tena...

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah anataka kulipwa mshahara mkubwa wa pauni 500,000 kwa wiki ili asaini mkataba mpya na Liverpool, kwa mujibu wa gazeti la The Mirror.

**Liverpool hivi karibuni ili wasainisha wachezaji wake wakubwa mikataba mipya, lakini bado majadiliano ya naendelea ili kumshawishi Salah kusaini kandarasi mpya.**

Nyota huyo wa kimataifa wa Misri mwenye umri wa miaka 29, awali aliripotiwa kwamba anataka kuondoka hapo Liverpool, huku klabu za Real Madrid na Barcelona zikionyesha nia ya kutaka kumsajili.

Mshindi huyo mara mbili wa Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora kwenye Ligi Kuu England amebakiwa na miaka miwili kwenye mkataba wake wa sasa na 'Wekundu' hao wa Anfield.

Virgil van Dijk, Alisson na nahodha, Jordan Henderson wote hivi karibuni walisaini mikataba mipya ya kuendelea kuichezea klabu hiyo.

Pia walinzi wa pembeni, Trent Alexander-Arnold na Andy Robertson wote wameshasaini mikataba mipya.

Na sasa Salah anataka alipwe pauni 500,000 kwa wiki ili aongeze mkataba wake hapo Anfield, akiwa ametua akitokea kule AS Roma Juni 2017.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Salah hatakuwa tayari kusaini mkataba mpya hadi pale atakapohakikishiwa kulipwa kiasi hicho. Na kama dili hilo litakubaliwa, Salah atakuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi katika historia ya Liverpool.

## ZISIKUPITE

### PSG YAFUNGUKA KWA RONALDO

KLABU ya Paris St-Germain ilizungumza na Cristiano Ronaldo kuhusu uhamisho kutoka Juventus msimu huu wa majira ya joto, lakini hakuna ofa yoyote iliyotolewa, na kumfanya mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 36, kurudi Manchester United. (***Goal***)

### LUKAKU NA MAFANIKIO INTER

ROMELU Lukaku mwenye umri wa miaka 28, amesema klabu yake ya zamani ya Inter Milan ilimtoa kwenye "shimo refu" baada ya kuondoka Manchester United mwaka 2019. Mshambuliaji huyo wa Ubelgiji alijiunga na Chelsea msimu huu wa majira ya joto. **(*Daily Mail*)**

### FODEN KUPEWA MKATABA

KLABU ya Manchester City itaongeza mara nne mshahara wa mchezaji wa England, Phil Foden mwenye umri wa miaka 21, wakati wanatafuta kumfunga klabuni hapo kwa kumpa mkataba mpya. (***Star***)

### CAMAVINGA NA REAL MADRID

REAL Madrid ilikuwa ikimfuatilia kiungo wa Ufaransa, Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 18, kwa miaka mitatu kabla ya kumsajili kutoka Rennes msimu huu wa majira ya joto. (***Marca***)

### TRAORE KUOTA MBAWA LIVER

MATUMAINI ya Tottenham Hotspur kumsajili winga wa Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 25, Januari yamepata pigo baada ya kufungua mazungumzo ya mkataba na klabu yake ya sasa ya Wolves. (***Express***)

### NEYMAR GHARAMA KUBWA

KUMSAJILI nyota wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 29, kutoka Barcelona mwaka 2017, kumeigharimu PSG pauni milioni 489 katika ada na mshahara wake. (***Marca***)

### RIBERY APATA TIMU

WINGA wa zamani wa Bayern Munich na Ufaransa, Franck Ribery, wiki hii atasaini mkataba na klabu ya Serie A, Salernitana. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 38, amekuwa huru tangu aondoke Fiorentina. **(*Fabrizio Romano*)**

### KESSIE AIKATALIA MILAN

KLABU za Tottenham Hotspur na Chelsea zimepewa tahadhari baada ya kiungo wa Ivory Coast, Franck Kessie mwenye umri wa miaka 24, kukataa mkataba mpya na AC Milan (***Gazzetta dello Sport***)

### KOEMAN HATIMULIWI BARCA

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta ana imani na kocha, Ronald Koeman na hana mpango wa kumtimua. (***Sport***)

## Kocha DTB ajivunia mastaa wa Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya DTB FC, inayoshiriki Ligi ya Championship (zamani Ligi Daraja la Kwanza), Ramadhan Nsanzurwimo, amesema usajili wa nyota wenye majina makubwa walioufanya, utaisaidia timu hiyo kucheza Ligi Kuu Bara msimu wa 2022/23.

DTB imesajili nyota wengi wenye majina makubwa waliowahi kupitia kwenye klabu kongwe na kubwa ndani na nje ya nchini akiwamo Yanik Bazola kutoka TP Mazembe ya DR Congo, Tafadzwa Kutinyu na Shafiq Batambuzi waliowahi kuitumikia Singida United ambayo iko Ligi Daraja la Pili.

Kipa Owen Chaima aliyewahi kuitumikia Mbeya City, David Mwantika ambaye aliwahi kukipiga Azam FC, Juma Abdul na Amis Tambwe wote waliwahi kuicheza Yanga na Yusuph Mlipili aliyewahi kuicheza Simba.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Nsanzurwimo alisema malengo yao makubwa ni kuipambania timu hiyo kufanya vizuri na kucheza Ligi Kuu msimu ujao wa 2022/23.

"Nina wachezaji wenye majina makubwa wamekubali kuja huku chini kwa sababu tu, wanahitaji kupata heshima kwa kupandisha timu kucheza Ligi Kuu, kulingana na kujulikana kwao nina matarajio makubwa sana na nyota hao kupambana na kutumia uzoefu wao kuhakikisha tunaenda kucheza Ligi Kuu msimu ujao wa 2022/23," alisema Nsanzurwimo.

## Klabu zakumbushwa kujitafutia wadhamini

**Na Saada Akida**

MTENDAJI Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), Almasi Kasongo, ametaja rasilimali fedha na miundombinu kuwa ni changamoto kubwa ambazo wanakutana nazo kila msimu, hivyo kuzitaka klabu kutobweteka hususan katika kutafuta wadhamini wao binafsi.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kasongo alisema katika suala la rasilimali fedha imekuwa shida kubwa na kutaka klabu kutotegemea udhamini wa jumla kutoka Shirikisho la Soka nchini (TFF), ambao wameupata na badala yake kila klabu kujitafutia wake binafsi ili kuweza kukabiliana na changamoto za kifedha.

Alisema suala la miundombinu linajulikana haliko upande wao, lakini anaamini viongozi wa klabu wakichangamka kutafuta wadhamini soka la Tanzania litakuwa kubwa.

"Ukiangalia changamoto hizi mbili, hasa rasilimali fedha, TPLB na TFF, wasipotafuta wadhamini basi kuna klabu zingine huwa zinakosa mdhamini na kutegemea hisani, klabu zimebweteka kujitafutia vyanzo vya mapato," alisema.

# DUCHU AMPAGAWISHA KOCHA BIASHARA UNITED

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Patrick Okumu, amesifu usajili wa David Kameta 'Duchu' ndani ya klabu hiyo kwa kueleza kuwa atakuwa msaada mkubwa kwao kwenye mechi za kimataifa kutokana na kipaji kikubwa alichonacho.

Kocha huyo raia wa Kenya, mbali na kusifu usajili wote uliofanywa na klabu yake, amesema amemwangalia Duchu kwa muda mfupi na kugundua kuwa ni kijana mdogo mwenye kipaji cha hali ya juu, huku tayari akiwa na uzoefu wa kucheza mechi za kimataifa, hivyo atakuwa msaada kwao.

"Usajili umefanyika vizuri, wachezaji wengi wamesajiliwa ni wazuri, hata huyu Duchu ambaye ametokea Simba, nimemwangalia ni mchezaji mdogo mwenye kipaji cha hali ya juu. Halafu ametoka klabu kubwa iliyokuwa inacheza mechi za kimataifa, yeye mwenyewe amecheza timu za taifa za vijana, hivyo ana uzoefu kwenye mechi za kimataifa na atatusaidia sana," alisema kocha huyo.

Okumu ameweka wazi kuwa alichogundua ni kwamba Tanzania ina wachezaji wengi wenye vipaji, lakini tatizo linakuwa ni kuviendeleza tu.

"Tanzania ina vijana wengi wenye vipaji sana, tatizo linakuwa ni kuviendeleza. Hapa ninao vijana kadhaa wa aina hiyo, nitakachofanya ni kuwaweka sawa ili kufanya vema kwenye mechi za Ligi Kuu na kimataifa," alisema.

**Duchu ambaye amejiunga na Biashara United kwa mkopo akitokea Simba, ameichezea timu hiyo kwa msimu mmoja, na amebakisha mkataba wa msimu mmoja.**

Biashara United msimu huu itaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika na itaanza na Dikhil ya nchini Djibouti, Septemba 10, mwaka huu.



Wachezaji wa Simba Queens wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika Uwanja wa Gymkhana jijini Nairobi, Kenya jana asubuhi, wakijiandaa kuwavaa Vihiga Queens katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake Ukanda wa CECAFA. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# *Simba Queens yapania fainali tiketi CAF*

**Na Somoe Ng'itu,** NAIROBI

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa upande wa Wanawake Ukanda wa CECAFA, Simba Queens ya Dar es Salaam, wanatarajia kuwakabili Vihiga Queens ya Kenya katika mechi ya hatua ya nusu fainali itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Nyayo jijini hapa.

Mchezo huo unatarajiwa kufanyika kuanzia saa 7: 00 mchana na utafuatiwa na mechi nyingine ya hatua ya nusu fainali itakaowakutanisha Commercial Bank of Ethiopia FC dhidi ya Mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Uganda, Lady Doves FC.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Hababuu Ali, ameliambia gazeti hili kuwa watacheza kwa kiwango cha juu kwa sababu wanahitaji kutinga fainali ya mashindano hayo.

Hababuu alisema watacheza kwa umakini na tahadhari kubwa ili kuhakikisha wanatimiza malengo yao ya kusonga mbele na hatimaye kubeba ubingwa wa michuano hii inayofanyika kwa mara ya kwanza.

Alisema wamejiandaa kukutana na ushindani katika mchezo huo kwa sababu wanafahamu wazi wapinzani wao pia wanaitamani tiketi ya kwenda kushiriki fainali za Afrika zitakazochezwa Novemba mwaka huu nchini Misri.

"Ni mechi ya kufa au kupona, sisi tunachagua ushindi tu na hatutaki kupata matokeo mengine, ushindi utatupeleka kwenye ndoto zetu, tumejipanga kukabiliana na ushindani katika mechi hiyo," Hababuu alisema.

Aliongeza kuwa wachezaji wake wote wako fiti na tayari kwa mchezo huo ambao utawaweka kwenye historia mpya endapo watatinga fainali.

Nahodha wa Simba Queens, Violeth Nicholas, alisema wamejiandaa kupeperusha vema bendera ya Tanzania katika mashindano hayo ambayo yameshirikisha timu tisa kutoka katika nchi tisa wanachama wa CECAFA.

"Tutahakikisha tunacheza kwa ajili ya kusaka ushindi, kwetu ni kama fainali, kila mchezaji amejipanga kucheza kwa kiwango cha juu na tutakuwa makini," nahodha huyo alisema.

Fainali ya mashindano hayo itafanyika Alhamisi, ikitanguliwa na mchezo wa kusaka mshindi wa tatu.

Michezo
Jumatatu Septemba 6, 2021
Nipashe



Salah ataka mzigo mrefu kusaini Liver
UKURASA 22

# NABI ATOA AGIZO ZITO KWA DIARRA, AUCHO

## ●●● Ni wakati wakivaana leo mechi ya kufuzu Kombe la Dunia kati ya Uganda na Mali, awataka kuhakikisha...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Klabu ya Yanga jana ikicheza mechi nyingine ya ndani ya mazoezi dhidi ya Pan African SC jana, kujiwinda na mchezo wa awali wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Nasreddine Nabi, amewataka mastaa wake waliopo timu ya taifa nje ya nchi kukwea pia mara moja pindi tu mechi yao kesho itakapomalizika.

Mbali na mechi moja ya kirafiki ya kimataifa iliyocheza Siku ya Kilele cha Mwananchi dhidi ya Zanaco FC ya Zambia na kupoteza kwa mabao 2-1, wiki iliyopita Yanga ilicheza mechi nyingine ya ndani ya kirafiki ya mazoezi dhidi ya Friends Ranger FC ya Manzese, Dar es Salaam na kushinda kwa mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Avic Town ilipo kambi yao.

Na jana jioni ilicheza mechi nyingine ya kirafiki ya mazoezi dhidi ya Pan African kwenye uwanja huo, lengo likiwa ni lile lile la kujiandaa mechi yao ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Rivers United ya Nigeria itakayopigwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema tayari Kocha Nabi, amewataka wachezaji wake wawili waliopo nje ya nchi kuzitumikia timu zao za taifa, kiungo Khalid Aucho wa Uganda na kipa Djigui Diarra kukwea pia mara moja pindi tu mechi yao itakapomalizika leo.

Uganda leo itaikaribisha Mali kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia nchini Qatar mwakani, na timu hizo zitakutana nchini Uganda baada ya mechi za awali Waganda kulazimisha sare tasa ugenini dhidi ya Kenya na Mali kuichapa Rwanda.

"Kwa ujumla maandalizi kuelekea mechi yetu ya kimataifa Jumapili, yanaendelea vizuri na wachezaji wote wapo fiti, hatuna majeruhi yeyote. Leo (jana) jioni tutacheza mechi nyingine ya mazoezi ya kirafiki dhidi ya Pan African ya Dar es Salaam.

"Kikubwa kocha alichoagiza ni kwa wachezaji wake wawili Aucho na Diarra, kuhakikisha wanaanza safari mara moja baada ya mechi yao ya kesho (leo) kumalizika ili kuwahi kuendelea na maandalizi na wenzao," alisema Bumbuli.

Kuhusu uwezekano wa kupata mechi nyingine ya ndani ama ya kimataifa ya kirafiki kujiandaa na mchezo huo dhidi ya Rivers United, Bumbuli alisema itategemea na maamuzi ya kocha lakini kwa sasa hajaagiza.

"Kwa upande wa mechi ya kimataifa ya kirafiki, hilo halipo kabisa kwa sababu siku ni chache haiwezekana kuanza kulishughulikia hasa ukizingatia wachezaji mpaka waanze kupimwa COVID-19 ili kupata kibali, hilo litakuwa ni vigumu, kama umelisikia hizo ni habari za mitaani tu hazina ukweli wowote.

"Lakini kama kocha atakuwa na mahitaji ya kupata mechi nyingine ya kirafiki ya ndani atatafutiwa ila bado hajasema," alisema Bumbuli.

Mbali na nyota hao wawili walipo nje ya nchi, wachezaji wengine wa Yanga ambao wanakosekana kambini ni Kibwana Shomari, Bakari Mwamunyeto, Dickson Job na Feisal Salum 'Fei Toto', ambao wapo nchini na timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars inayojiandaa kuikaribisha Madagascar katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia nchini Qatar 2022.

**TUPO TAYARI...**



Wachezaji wa Taifa Stars, Mohamed Hussein 'Tshabalala' (mbele), Simon Msuva (kushoto) na Erasto Nyoni wakiwa mazoezini Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, kujiandaa na mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia 2022 dhidi ya Madagascar itakayopigwa uwanjani hapo kesho. **PICHA: TFF**

## Okwi atangaza kurudi Simba SC

**Na Somoe Ng'itu, NAIROBI**

MSHAMBULIAJI na Nahodha wa Timu ya Taifa ya Uganda (Cranes), Emmanuel Okwi, amesema anaamini ipo siku atarejea kwa mara nyingine kwa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania, Simba ya jijini Dar es Salaam.

Okwi ambaye aliwahi kuichezea Yanga ya Tanzania, kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake na Al-Ittihad ya Misri tangu Juni 30, mwaka huu.

Mshambuliaji huyo alikuwa jijini hapa Ijumaa iliyopita akiiongoza Cranes katika mchezo wa Kundi E wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar dhidi ya Kenya ambao ulichezwa Jumamosi iliyopita na kumalizika kwa sare ya bila kufungana.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa, Okwi alisema bado yuko katika kiwango cha juu na nafasi ya kurejea kucheza soka la kulipwa Tanzania ipo endapo atafikia makubaliano na klabu yoyote.

Okwi alisema kwa sasa ameielekeza akili na nguvu yake kuisaidia Uganda ifanye vizuri kwenye mashindano hayo na anaamini watapambana kuhakikisha wanatimiza malengo yao.

"Naamini siku moja nitarejea Simba, ni suala la muda," alisema kwa kifupi mshambuliaji huyo wa zamani wa SC Villa ya Uganda.

Aliongeza kuwa anafurahi kuona amekutana tena na Kocha Mserbia Milutin Micho katika kikosi cha Uganda na wameanza vema kwenye kampeni hiyo ya kuelekea Qatar.

"Ni kocha ambaye anaifahamu vema Uganda, naamini atatumia uzoefu wake kutufikisha mbali, akiwa nje amejifunza mambo mengi ambayo yatasaidia kukiimarisha kikosi chetu cha Uganda," Okwi alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >